# KUCHUNGUZA JINSI NAHAU ZA KISWAHILI SANIFU ZINAVYOKWAMISHA MAWASILIANO FANISI KWA WAGENI WA LUGHA

**MWANAISHA MUSSA SKUNI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA KUKAMILISHA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

# ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo "Kuchunguza jinsi Nahau za Kiswahili Sanifu zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lugha" na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti la kutunukiwa Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

--------------------------------

**Dr. Mohamed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

…………………….…..

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga, kunakili kwa namna yoyote na kwa lengo lolote tasnifu hii bila ya idhini ya mmiliki au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba

# TAMKO

Mimi **Mwanaisha Mussa Skuni**, natamka kwamba tasnifu hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine Chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine yoyote.

……………………..

Sahihi

……………………..

Tarehe

## TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wawili Bw.Mussa Skuni Juma na Bibi Safia Nassor Rashid kwa kunilea kwa mapenzi ya hali ya juu. Pia ninaitabaruku kwa watoto wangu; Ummukulthum Iddi moh'd, Suleiman, Yussra, Maryam, Aisha, Mussa, Muhiddin na Rahila . Vile vile ninaitabaruku kwa walezi wangu Bw. Mmanga mgeni Na Bibi Rukia Mussa kwa kunilea kwa moyo wa upendo uliochanganyika na huruma pamoja na kunipeleka shule kupata elimu na kunikuza katika maadili mema ya kiislamu ambayo ndiyo dira ya maisha yangu ya hapa duniani na huko akhera .

## SHUKURANI

Awali ya shukurani zangu nazipeleka kwa muumba wa ardhi na mbingu na vyote vilivyomo ndani yake kwa kunijaalia kuwa mwenye akili timamu, nguvu, afya njema, uwezo na maarifa, ustahamilivu , uvumilivu na utulivu wa moyo katika kipindi chote cha masomo yangu haya ya uzamili na kwa hili ninakiri wazi wazi kwamba sio kwa uwezo , uhodari, wala ujanja wangu ila ni kwa idhini yake yeye ALLAH (SW) Hivyo shukurani hizo nazipeleka kwake ingawa kwa kusema Alhamdulillah Rabbil-Alamina. Pili napenda kumshukuru kwa udhati wa moyo wangu msimamizi wangu Dr. Mohamed Omary Maguo kwa kukubali kuwa msimamizi wangu ambapo aliniongoza na kunielekeza kuanzia hatua ya kwanza hadi kufikia tamati ya utafiti huu Mungu ambariki. Tatu shukurani zangu zisizo na mfano zimwendee mwalimu wangu mlezi Bw Bakar Kombo Bakar kwa muongozo, maelekezo, na ushauri alioweza kunipa ambao una thamani kubwa katika maisha yangu . Na hii ni dalili ya wazi wazi kwamba bila ya usimamizina uelekezi wake isingeweza kufikia katika hatua hii kwa wakati huu. Hivyo kwa upendo na unyenyekevu mkubwa namuomba ALLAH (SW) amjaalie kila la kheri pamoja na afya njema na aukuze moyo wake wa imani na ujasiri wa kuwatakia mema wenzake, ampe umri mrefu na ajaalie uwe na manufaa kwake ili aweze kuendelea kuwa hazina kubwa inayotegemewa na kufaa kizazi kilichopo sasa na kinachofuata baadae. Nne shukurani za pekee zimwendee mume wangu mpenzi Bw. Iddi Moh’d Juma kwa kuniruhusu kusoma masomo haya ya uzamili. Pia kunipa maelekezo na kunitia moyo wakati nilipokuwa nakata tama kutokana na ugumu wa kazi hii ya utafiti nae namuomba ALLAH ambariki na ampe kila la kheri. Pia nawashukuru wazazi wangu Bw. Mussa Skuni Juma na Bibi Safia Nassor Rashid na walezi wangu Bw. Mmanga

Mgeni na Bibi Rukia Mussa kwa kunilea katika maadili mema ya kiislamu na kunipeleka shule kupata elimu. Vile vile naishukuru familia yangu kuvumilia na kustahamili tabu na shida walizokuwa wakipambana nazi kipindi chote cha masomo yangu haya na kuyakosa malezi ya mama yao mzazi ambayo ni muhimu sana kwao. Kwa hili namuomba Mungu awajaalie dini iliyojaa imani, awaelekeze katika njia iliyonyooka , na mimi niwe kegezo chema kwao cha kufuata katika kutafuta elimu yenye manufaa kwa hapa duniani na huko akhera. Pia shukurani za dhati zimwendee Machano Mmanga Mgeni kwa kutoa mchango wake mkubwa katika utafiti huu. Mungu amzidishie imani.Vile vile nitakuwa mwizi wa fadhila nikiwacha kuwashukuru wakuu wangu wa kazi akiwemo mwalimu wangu mkuu kwa kuniruhusu pale ninapoomba ruhusa kwao. Na mwisho napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu Maryam Rashid Ali, Zaitun Hassan Sheha, Miza Hassn Faki, Amina Makame Haji, Riziki Ali Hamad, Aisha Ameir Moh’d, Bishara Nassor Moh’d, Bimkuwa Abdalla Hamza na Fatma Hamad Nassor kwa kunisaidia kwa njia moja au nyengine nasema Ahsanteni sana.

## IKISIRI

Utafiti huu unalenga“Kuchunguza jinsi Nahau za Kiswahili zinavyokwamisha Mawasiliano kwa Wageni wa Lugha”. Nahau hizo zinatumika katika lugha ya maandishi ya Kiswahili na katika mazungumzo ya kila siku. Mtafiti wa utafiti huu aliongozwa na malengo mahsusi matatu ambayo ni kubainisha nahau mbali mbali za lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia makundi yake kimuktadha, kuchambua maana ya nahau Kipragmatiki na maana ya nahau kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau hizo (Kisemantiki), na kubainisha jinsi nahau zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha. Utafiti huu umefanyika katika kisiwa cha Pemba, katika hospitali ya Wete,hopitali ya wakorea Chake chake na hospitali ya Abdalla Mzee na katika Mtaa wa Mkoroshoni Chake chake. Pia utafiti hu ulifanyika shule ya sekondari ya Uweleni na shule ya sekondari ya Utaani na Chuo Cha Kiislamu Pemba Mbinu ya uwandani na maktabani zilitumika katika kufanya utafiti huu na njia zilizotumika ni dodoso, mahojiano . Sampuli iliyotumika ni ya wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili wa shule zilizoteuliwa. Mtafiti alitumia nadharia ya maana katika matumizi na nadharia ya maana katika muktadha. Matokeo ya jumla ya utafiti huu yanaonyesha kuwa lugha ya kiswahili ni pana katika matumizi yake. Pia mtafiti amegundua kuwa mambo yanayopelekea matumizi ya nahau yasababishe kufeli kwa mawasiliano kwa wageni wa lugha ni pamoja na wageni kujifunza zaidi sarufi ya lugha na kuiwacha kabisa kabisa fasihi ya lugha.Vile vile Nahau hazitoi maana kisarufi. Hata hiyo matokeo yanaonyesha kuwa nahau hazikwamishi mawasiliano kwa wageni wa lugha tu bali pia na wazawa wa lugha wanakabiliwa na taizo hili.

## YALIYOMO

**ITHIBATI** ........................................................................................................ **ii**

**HAKIMILIKI** ...................................................................................................... **iii**

**TAMKO** ............................................................................................................. **iv**

**TABARUKU** ....................................................................................................... **v**

**SHUKURANI** ..................................................................................................... **vi**

**IKISIRI** ............................................................................................................... **viii**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ............................................................................. **xv**

**ORODHA YA VIFUPISHO** ................................................................................ **xvi**

**SURA YA KWANZA** .......................................................................................... **1**

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA** ........................................................................... **1**

1.1 Utangulizi wa Sura ........................................................................................... 1

1.2 Usuli wa Tatizo ................................................................................................ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ................................................................................................ 3

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................... 5

1.4.1 Lengo Kuu ..................................................................................................... 5

1.4.2 Malengo Mahususi ........................................................................................ 5

1.5 Maswali ya Utafiti ........................................................................................... 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................ 6

1.7 Vikwazo vya Utafiti ......................................................................................... 6

1.8 Utatuzi wa Vikwazo ......................................................................................... 7

1.9 Hitimisho ......................................................................................................... 7

**SURA YA PILI** ................................................................................................... **9**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA** ....... **9**

2.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi ........ 9
2.2 Kazi Tangulizi Zinazohusiana na Semi ........ 10
2.2.1 Dhana ya Semi ........ 10
2.2.2 Vipera vya Semi ........ 12
2.3 Dhana ya Maana ........ 15
2.3.1 Maana katika Mtazamo wa Kisemantiki ........ 15
2.3.2 Maana katika Mtazamo wa Kipragmatiki ........ 15
2.4 Kazi Tangulizi kuhusu Semi ........ 16
2.5 Pengo la Utafiti ........ 18
2.6 Kiunzi cha Nadharia ........ 19
2.6.1 Maana ya Nadharia ........ 19
2.6.2 Nadharia ya Maana ya Matumizi ........ 20
2.6.3 Nadharia ya Maana Kimuktadha ........ 21
2.7 Hitimisho ........ 22
**SURA YA TATU ........ 23**
**3.0 MBINU ZA UTAFITI ........ 23**
3.1 Utangulizi wa Sura ........ 23
3.2 Muundo wa Utafiti ........ 23
3.3 Kundi Lengwa ........ 23
3.4 Sampuli ........ 24
3.5 Usampulishaji ........ 24
3.6 Maana ya Data ........ 25
3.6.1 Aina za Data ........ 25
3.7 Mbinu za Kukusanyia Data ........ 26

3.7.1 Dodoso .......... 27
3.7.2 Mahojiano .......... 27
3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data .......... 28
3.9 Maadili ya utafiti .......... 29
3.10 Hitimisho .......... 30
**SURA YA NNE .......... 31**
**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA .......... 31**
4.1 Utangulizi wa Sura .......... 31
4.2 Kubainisha Nahau za Kiswahili kwa Kuzingatia Makundi .......... 33
4.2.1 Tafsiri ya Matokeo .......... 34
4.2.2 Nahau zinazohusu Mila na Desturi za Jamii .......... 35
4.2.3 Nahau Zinazohusu Juhudi katika Kazi .......... 37
4.2.4 Nahau zenye Uhusiano wa Dini na Imani .......... 37
4.2.5 Nahau Zimazohusu Choyo na Usaliti .......... 38
4.2.6 Nahau Zinazohusu Subira na Uvumilivu .......... 38
4.2.7 Nahau Zinazohusiana na Mambo ya Maadili .......... 39
4.2.8 Nahau Zinazohusu Ushirikiano .......... 39
4.2.9 Nahau Zinazohusu Elimu .......... 39
4.3 Kuchambua Maana ya Nahau Kipragmatiki na kwa Kuzingatia Viambajengo vilivyounda Nahau hizo .......... 39
4.3.1 Kuchambua Maana ya Nahau Kipragmatiki .......... 41
4.3.2 Tafsiri ya matokeo .......... 43
4.3.3 Kuchambua Maana za Nahau kwa Kuzingatia Viambajengo Vilivyounda Nahau .......... 44

4.4 Kubainisha jinsi Nahau zinavyokwamisha Mawasiliano kwa Wageni wa Lugha ya Kiswahili ........ 46
4.4.1 Nahau “ Amevunja Chupa” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili ........ 47
4.4.2 Nahau “Kuchimba Dawa” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili ........ 48
4.4.3 Nahau “Amepata jiko” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili ........ 49
4.4.4 Nahau “Jamvi la Wageni” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ........ 50
4.4.5 Nahau “Amepata Ua” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ........ 50
4.4.6 Nahau “Kenda Kombo” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ........ 51
4.4.7 Nahau “Andika Meza” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ........ 52
4.4.8 Nahau “Kuchungulia Kaburi” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ........ 52
4.4.9 Nahau “Amevunja Ungo” Inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ........ 53
4.4.10 Nahau “Ameacha njia” Inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ........ 54
4.4.11 Nahau “Aliniunga Mkono” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ........ 54

4.4.12 Nahau “Ameanguka mtungi” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ... 55
4.4.13 Nahau “Kutapikia sandani ” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ... 56
4.4.14 Nahau “Amaemlanda baba yake” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ... 57
4.4.15 Nahau “ Ameukata” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa ... 57
4.4.16 Nahau “ Bao la Mkahawani”inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili ... 58
4.4.17 Nahau “ Kata maini” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili ... 58
4.4.18 Nahau “Chomea utambi” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili ... 59
4.4.19 Nahau “Kaza buti” ” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili ... 60
4.4.20 Nahau “Ana Ndimi Mbili” Inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ... 60
4.4.21 Nahau “Kujipalia Makaa” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ... 61
4.4.22 Nahau “Kupigwa fyagio la chuma” inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ... 61
4.5 Hitimisho la Sura ... 62
**SURA YA TANO ... 64**
**5.0 MUHUTASARI HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... 64**

5.1 Utangulizi .......... 64
5.2 Muhtasari wa Utafiti .......... 64
5.3 Matokeo ya Utafiti kwa Kila Lengo .......... 65
5.3.1 Lengo la Kwanza .......... 65
5.3.2 Lengo la Pili .......... 65
5.3.3 Lengo la Tatu .......... 66
5.4 Matokeo ya Jumla .......... 67
5.5 Mchango wa Utafiti .......... 68
5.6 Mapendekezo kwa Tafiti Fuatishi .......... 68
5.7 Hitimisho .......... 69
**MAREJELEO .......... 70**
**VIAMBATANISHO .......... 73**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jeduweli Na :4.1: Watafitiwawa Kigeni ... 32

Jeduwali Na.4.2: Watafitiwa Wanafunzi ... 32

Jeduwali Na. 4.3: Watafitiwa Walimu ... 32

Jeduwali Na. 4.4: Mgawanyiko wa Majibu ya Watafitiwa ... 34

Jeduwali Na 4.5: Makundi ya Nahau Zilizobaininishwa ... 35

Jeduweli Na 4.6: Maana ya Nahau Kipragmatiki ... 41

Jeduweli Na. 4.7: Mfano wa Nahau Katika Kiwango Cha Neno ... 42

Jeduweli Na. 4.8: Mfano wa Nahau Katika Kiwango Cha Kirai ... 43

Jeduwali Na 4.9: Maana ya Nahau Kwa Kuzingatia Viambajengo Vilivyounda Nahau ... 45

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKITA | Baraza la Kiwahili Tanzani |
| N | Nahau |
| Na | Nambari |
| Sn | Serial number |
| SW: | Subhana Wataala |
| T | Tafsiri |
| TAKILUKI | Taasisi ya kiwhili na lugha za kigeni |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiwhili |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiwhili |
| TUMI | Taasisi ya Ukuzaji Mitaala |
| UK | Ukurasa |
| UKIMWI | Ukoefu wa Kinga Mwilini |
| W KE | Wanawake |
| WU | Wanaume |

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii inatoa taarifa za awali zinazohusiana na mada ya utafiti ambayo ni "Kuchunguza jinsi Nahau za Kiswahili zinavyokwamisha Mawasiliano kwa Wageni wa Lugha". Sura hii imeundwa na sehemu kumi. Sehemu ya kwanza inaeleza utangulizi wa jumla kuhusu mada ya utafiti. Sehemu ya pili inatoa taarifa kuhusu usuli wa tatizo la utafiti. Sehemu ya tatu inaeleza tatizo la Utafiti. Sehemu ya nne inaeleza pengo la utafiti. Sehemu ya tano inaeleza malengo. Sehemu ya sita ni maswali ya utafiti, sehemu ya saba ni umuhimu wa utafiti. Sehemu ya nane inahusu changamoto za utafiti na jinsi ya kutatua changamoto hizo na sehemu ya tisa inaeleza hitimisho la sura hii.

## 1.2 Usuli wa Tatizo

Kihistoria, Kiswahili ni miongoni mwa lugha ambazo hukua na kupokea mabadiliko tofauti (Masamba 2006). Katika karne tulizonazo wanaisimu wa lugha ya Kiswahili pamoja na watumiaji wengine wa lugha hiyo wameshuhudia mabadiliko makubwa ya lugha ya Kiswahili kutokana na kuongezeka kwa idadi ya semi, nahau ikiwa ni miongoni mwao. Inasadikiwa kuwa idadi kubwa ya wageni wanaotumia Kiswahili wamekabiliwa na tatizo la matumizi ya nahau katika matumizi yao ya lugha hii, jambo ambalo hupelekea ugumu mkubwa kimawasiliano. Kiisimu, hakuna anayekataa kuwa kuongezeka kwa idadi ya nahau katika lugha ya Kiswahili ndiko kunakopelekea kuibuka kwa tatizo la ugumu wa kujifunza lugha kwa wasiokuwa

wazawa wa lugha hii (Kitiso 1988). Licha ya jitihada mbali mbali za kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inapata watumiaji wengi duniani na kuikuza hadhi yake kuwa ni lugha ya kimataifa, bado majibu ya tatizo la kuibuka kwa nahau zinazosababisha ugumu wa kujifunza lugha hiyo kwa wageni ni kitendawili kinachohitaji kuteguliwa (BAKIZA, 2008). Kuna kazi nyingi zilizoandikwa kuhusiana na mada ya semi za Kiswali nahau zikiwemo. Mfano wa kazi hizo ni ile ya (Kiiza (2004), ambaye aliandika kuhusu jinsi semi za Kiswahili zinavyozaliwa na kukua katika Lugha ya Kiswahili na aligundua kuwa baadhi ya semi huzaliwa, hukuwa na kufa, kutegemeana na mabadiliko ya wakati na mahitaji ya watumiaji wa lugha . Mbunda (1992) alifanya utafiti juu ya namna gani nahau zinavyotumika katika lugha ya Kiswahili na alithibitisha kuwa nahau zinatumika kuipamba lugha na kupunguza ukali wa maneno. Kwa upande mwengine Balisidya (1976) yeye alitafiti juu ya umuhimu wa nahau zinazoibuka katika maendeleo ya Kiswahili na kugundua kuwa nahau zina umuhimu mkubwa katika kukuza lugha kwani husaidia kuibua misamiati mipya katika lugha.Kiukweli, pamoja na jitihada za watafiti hawa, mtafiti wa kazi hii anaona ipo haja ya kuchunguza zaidi kwa sababu maandiko yote aliyoyabainisha hapo juu hayajamuonesha andiko mahsusi lililolenga katika kuchunguza jinsi nahau za Kiswahili zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha. Waandishi walio wengi walizungumzia vipengele vyengine vya nahau hasa vile vinavyohusiana na uchambuzi wa kifasihi na bado hawajachunguza kipengele kinachohusiana na nahau kwa kuangalia mtazamo wa Kiisimu. Kwa msingi huu, mtafiti wa kazi hii anakusudia kufanya utafiti katika kuchunguza jinsi nahau za Kiswahili Sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi kwa wageni wa lugha ili kutoa andiko mahsusi ambalo litasaidia kwa namna tofauti kufahamu jinsi hali hii

inavyokwamisha mfumo wa mawasiliano kwa wageni wa lugha hiyo jambo ambalo husababisha kupungua kwa ufanisi wa mawasiliano kwa watumiaji wapya wa lugha ya Kiswahili.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Kutokana na tafiti rejelewa na maandiko mbali mbali yaliyokwisha wasilishwa juu ya semi za Kiswahili, mtafiti wa mada hii anakiri wazi wazi kuwa kuna tafiti nyingi zilizokwishafanywa juu ya mada ya semi katika vipengele mbali mbali. Kwa mfano Mahenge (2009) alichunguza semi zilizoandikwa kwenye tiketi za daladala jijini Dar es salaam. Katika utafiti wake aliangalia kipengele cha fani na maudhui . Migodella (2011) alichunguza ufasihi wa misemo au semi ziliziandikwa katika sehemu za umma, akitolea mifano misemo iliyoandikwa katika kuta za vyoo. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kwamba semi zilizoandikwa katika kuta za vyoo zina utajiri mkubwa wa matumizi ya lugha ya kitamathali kama vile tashbiha, tafsida, sitiari, taswira, ishara, picha nakadhalika. Uledi (2012) nae alichunguza muundo wa vipengele vya lugha katika methali na vitendawili kwa jamii ya wamakunduchi. Kazi yake ilikuwa ni kulinganisha semi hizo na zile za Kiswahili sanifu na kugundua kuwa katika kila methali na vitendawili kuna vipengele mbali mbali vya lugha vinavyotumika katika ujenzi wake. Hassan (2013) alichunguza dhima za methali katika jamii ya Wapemba na kubaini kwamba methali zinatumika katika jamii ya Wapemba kwa kuangalia dhima ya methali ili kudumisha dhamira na maadili katika jamii. Vile vile Alhabib (2012) alichunguza matumizi ya taswira katika nyimbo za taarab na kugundua kuwa kipengele cha misemo kinajidhihirisha katika nyimbo za taarab .Vile vile Rajab (2012) alifanya utafiti juu ya dhima za misemo iliyoandikwa

katika fulana, ambapo alishughulikia zaidi kipengele cha dhamira na matumizi ya lugha katika jiji la Dar es salaam. AIichogundua ni kwamba maandishi yaliyoandikwa katika vazi la fulana yamejaa dhamira mbali mbali, alitaja baadhi ya dhamira hizo kuwa ni umaskini, hali ngumu ya maisha, UKIMWI, dini, elimu, chuki, maisha, wivu, pesa, umuhimu wa kufanya kazi, vita dhidi ya magonjwa. Nassor (2016) akafanya utafiti juu ya kuchunguza fani na dhamira za semi zilizoandikwa katika vyombo vya safari vya baharini kisiwani Pemba. Katika kazi yake hiyo aligundua kuwa katika semi zilizoandikwa katika vyombo vya safari zimetumika mbinu mbali mbali za kisanaa kama vile tashtiti, taswira, kejeli, methali, misemo, simo, misimu nakadhalika .Vile vile aligundua kuwa dhamira inayotumika katika semi hizo ni dhamira ya maisha ya kila siku pamoja na maisha ya baadae huko akhera. Dhamira hizo ziliwasilishwa na kujitokeza katika semi zilizoandikwa katika vyombo vya baharini kisiwani Pemba. Tafiti zote hizo kwa kiasi anachoelewa mtafiti wa kazi hii bado hazijabainisha ni kwa kiasi gani semi kupitia kipengele cha nahau zinavyokwamisha mfumo wa mawasiliano kwa wageni wa lugha ya Kiswahili. Kama hivyo ndivyo ilivyo, basi mtafiti amebaini kuwa bado wanaisimu wa Kiswahili hawajawahi kuweka bayana namna gani nahau za Kiswahili zinavyokwamisha mfumo wa mawasiliano kwa wageni wa lugha hiyo. Kwa maana hiyo, mtafiti wa kazi hii amelazimika kuichagua mada hii ili wadau wa isimu ya Kiswahili waweza kufahamu kwa kuweka bayana namna nahau zinavyokwamisha mfumo wa mawasiliano kwa wageni wa lugha hiyo. Utafiti huu umekuwa ni wa lazima kufanywa kwa lengo la kupata andiko mahsusi lenye sifa za kipekee na lenye kutafautiana na maandiko mengi yaliyotolewa na wataalamu ambalo litasaidia katika kupunguza tatizo la kutokufahamu namna nahau za Kiswahili sanifu

zinavyokwamisha mfumo wa mawasiliano kwa wageni wa lugha hiyo. Hii inatokana na ukweli kwamba wakati wa mapitio ya maandiko mbali mbali mtafiti hakubahatika kuona andiko mahasusi ambalo linazungumzia juu ya mada kama hii.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na malengo yafuatayo:-

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza jinsi Nahau za Kiswahili Sanifu zinavyokwamisha aawasiliano fanisi kwa wageni wa lugha.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Kwa ajili ya kukamilisha lengo kuu lililoanishwa hapo juu, utafiti huu umejumuisha malengo mahsusi yafuatayo:-

i) Kubainisha nahau mbali mbali za lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia makundi yake.
ii) Kubainisha maana ya nahau kipragmatikia na maana ya nahau kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau hizo (kisemantikia).
iii) Kubainisha jinsi nahau zinavyokwamisha mawasililiano kwa wageni wa lugha.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu una jumla ya maswali matatu ambayo yalimuongoza mtafiti kukamilisha au kufikia malengo yake ya utafiti. Kila swali linahusiana na lengo mahsusi moja. Maswali hayo ni kama yafuatayo:-

i) Ni zipi nahau za lugha ya Kiswahili?

ii) Ni maana zipi za kipragmatikii na maana zipi za kisemantiki za nahau za Kiswahili Sanifu?

iii) Ni jinsi gani nahau za Kiswahili zinakwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Kwanza kabisa, utafiti huu unatarajiwa kutumika kama chanzo cha maarifa kinachooonesha jinsi gani nahau za Kiswahili zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha. Pili, utafiti utaweza kutumiwa na wataalamu wa lugha, isimu na wengineo kama chanzo cha maarifa au kama marejeleo kwa ajili ya tafiti za baadaye ama kwa kurekebisha au kukosoa kazi hii. Pia, hivi sasa lugha hii ipo katika mchakato wa kuwa lugha ya mawasiliano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla, wakati miongoni mwa sifa za lugha ni kuwa na watumiaji wengi. Hivyo, utafiti huu utawasaidia wanaisimu wa lugha ya Kiswahili katika kutatua tatizo la ugumu wa kujifunza lugha linalosababishwa na kuibuka kwa Nahau za Kiswahili. Mwisho, utafiti huu utakuwa ni rejeleo muhimu ambalo litatumiwa na wahadhiri pamoja na wanafunzi wao wa shahada za awali, uzamili na uzamivu. Kwa upande wa wahadhiri utafiti huu utawawezesha kuandaa mihadhara yao juu ya masuala ya nahau za Kiswahili na jinsi zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti

Katika utafiti huu mtafiti alikutana na vikwazo tofauti ambavyo kwanza kabisa mtafiti ni mtumishi wa serikali tena ni mwalimu ambae ana majukumu ya

kufundisha wanafunzi kwa wakati maalumu hivyo mbali na kazi yake hii alilazimika ahakikishe anakamilisha kazi zote za mwaka mzima kama ambavyo kanuni za kazi yake zinavyomtaka . Pia kwa vile walengwa wa utafiti huu walikuwa ni walimu na wanafunzi mtafiti aliweza kupata shida ya kukusanya data kwa kiasi fulani kwa walengwa husika kwani mara nyengne aliwakuta wakiendelea na masomo kama ratiba zao zinavyoelekeza kitu ambacho kiliweza kumsababisha mtafiti apoteze muda kwa kusubiri hadi kumaliza vipindi vyao vya masomo na wakati mwengine kuwakosa kabisa

## 1.8 Utatuzi wa Vikwazo

Mtafiti wa utafiti huu aliweza kutatua vikwazo vilivyomkabili kama ifuatavyo :- Kwa upande wa majukumu ya kazi mtafiti aliandaa utaratibu mzuri wa kuwafundisha wanafunzi wake kwa wakati muafaka ikiwa ni pamoja na kuwapangia muda wa ziada pindi ilipotokezea kuwakosa katika wakati wa kawaida. Kwa upande wa upatikanaji wa walengwa mtafiti alifanya jitihadaza maksudi kuwasubiri hadi walipomaliza masomo yao na kwa wale aliowakosa kabisa ilimbidi arudi tena kwa siku nyengine kitu ambacho kilipoteza muda mwingi na gharama za mtafiti kwa sababu maeneo mengine aliyoyafanyia utafiti yalikuwa yako mbali nae.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii ni ya utangulizi wa utafiti mzima ambapo vipengele mbalimbali vya kiutangulizi vimewasilishwa. Miongoni mwa vipengele hivyo ni pamoja na utangulizi wa jumla, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake. Vipengele vyote

hivi kwa pamoja vimetusaidia katika kupata uhalali wa kufanyika kwa utafiti wetu. Tunayasema haya kwa sababu katika vipengele hivi ndimo tatizo la utafiti lilipobainishwa. Sura inayofuata inafanya upitiaji wa maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti wetu

# SURA YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

Hii ni sura inayohusu mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia. Katika sura hii kuna mambo mawili makubwa yaliyojadiliwa. Mambo hayo ni pamoja na mapitio ya kazi tangulizi na la pili ni ufafanuzi wa kiunzi cha nadharia.

### 2.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Cozby (2012) anasema kwamba kazi tangulizi ni makala zote zinazofupisha tafiti katika eneo fulani. Cozby anaendelea kusema kupitia maandiko ni mchakato unaohusu uchunguzi wa kina wa maandiko yaliyotangulia katika eneo fulani la taaluma. Kazi tangulizi zinaweza kuwa vitabu, makala au majarida. Lengo la kupitia kazi tangulizi ni kubainisha tafiti zilizofanyika kuhusiana na eneo husika zimefanyikaje, kupata mwamga wa jinsi kazi ya utafiti inavyowasilishwa mwanzo hadi mwisho na kubainisha pengo lililoachwa na watafiti waliotangulia ili liweze kupunguza mwanya uliopo. Mapitio ya kazi mbali mbali hutoa muongozo kwa mtafiti. Mchakato mzima wa kupitia kazi mbali mbali hufungamana na kanuni zake kama kuhakiki kujadili na kutoa maoni ya mtafiti ili kuimarisha zaidi utafiti unaofanywa. Enon (1998:41) anasema kwamba, mapitio ya kazi tangulizi ni mpangilio maalumu wa ufafanuzi na uchambuzi wa maandishi kuhusu habari inayohusiana na suala la utafiti. Enon ameendelea kusema kwamba, mpitio ya kazi tangulizi yanaweza kuwa vitabu, makala, majarida mbali mbali na vyanzo vyengine vinavyotoa muongozo kwa mtafiti kuweza kugundua pengo ambalo linahitaji kuzibwa.Vile vile Enon (keshatajwa) amesema mapitio ya kazi tangulizi ni maarifa

yanayopatikana kwa kuzamia mbizi maandishi yaliyopita huko nyuma ambayo hufananishwa na taarifa hai yaliyopatikana ndani ya utafiti mpya. Katika uzamiaji huu wa kutalii kazi tangulizi yanayoibuliwa ni pamoja nadharia zinazotumika katika kuchambua data.

## 2.2 Kazi Tangulizi Zinazohusiana na Semi

### 2.2.1 Dhana ya Semi

Ijapokuwa utafiti huu unashughulikia nahau, mtafiti ameona ni vyema kwanza kufafanua dhana ya semi, kwani nahau inatokana na semi na bila ya semi nahau zisingekuwepo. Imekuwa semi ni kama mzazi na nahau ni mtoto na katika hali ya kawaidia bila ya mzazi mtoto hapatikani. Wataalamu waliozungumzia semi ni pamoja na Balisidya (1979),Ngole na Honero (1982), Mlacha(1985), Mbunda (1992:48), Mulokozi (1996:35) Wamitila (2003:135),Mbonde (2005), Mturo(2011), Wataalamu wote hawa wamekubaliana kwamba "Semi ni utanzu miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi" Wao wamezifasili semi kuwa ni kauli au tungo fupi fupi zinazobeba misemo pamoja na mafumbo yanayopelekea kupatikana kwa mafunzo katika jamii. Wataalamu hawa wamezigawanya semi kama ifuatavyo:-

Mulokozi (1996) amezigawanya semi kuwa ni methali, mafumbo, vitendawili, misimu, lakabu, na kauli tauria. Balisidya (1979) amezigawa semi katika makundi matatu nayo ni misimu, vitendawili na methali, kisha akazigawa semi katika vipera vidogo vidogo mfano katika methali kuna nahau na misemo na katika vitendawilil kuna vitendawili na mafumbo. Ngole na Honero (1982) wameeleza vigezo vinavyotafautisha methali na misemo ni uzito wa agizo au adili anayopata binadamu.

Usemi ambao hautoi agizo au adili maalumu unaitwa misemo na usemi ambao unatoa agizo au adili kwa binadamu unaitwa methali. Imezoeleka kuwa semi katika Kiswahili zinatumia picha mbali mbali kama vile ndege wanyama, mimea na viumbe vyengine. Lengo la picha hizo ni kuwakilisha binadamu. TUKI (1990) wao wanasema semi ni fungu la tungo za fasihi ambazo ni fupi fupi zenye kutumia picha tamathali na ishara. Fungu hilo lina tanzu kama vile misemo ambayo husemwa kuwa ni tungo zitumiazo picha, ishara na tamathali kueleza kitu au wazo kwa ufupi, ili litolewe maadili au maonyo fulani. Katika kazi yao hiyo misemo inaonyesha kumithilishwa na matukio au vitu. Mfano “Mtoto wa nyoka ni nyoka.” Kuhusu mafumbo wameeleza kuwa utanzu huu una vijitanzu vya vitendawili na mizungu. Vitendawili ni semi fupi fupi za fumbo zenye kutumia picha tamathali na ishara kueleza wazo lililofichika ambalo ndilo jawabu la fumbo. Mizungu ni vitendawili vinavyotumiwa katika miviga kueleza dhana na mawazo mbali mbali kwa maongezi au katika nyimbo. Mfano wa fumbo walilotoa ni “Miti yote nitakwea, mtarawanda unanishinda”. Misimu wanasema ni semi ndogo ndogo za kupita ambazo huzushwa katika mazingira fulani na baadae hutoweka. Mlacha (1985) ameieleza semi katika kipera cha methali kwa kuitaja kuwa ni sentensi yenye sura kama methali yenye muundo wa kipekee ambao hutofautisha methali na sentensi nyengine. Methali ni fupi na zimekamata matendo mapana sana yanayoweza kufafanulika kwa maneno ya kawida. TUMI (1990) wao wana maoni kuwa semi ni fungu la tungo za fasihi ambazo ni fupi fupi zenye kutumia picha, tamathali na ishara. TUMI (weshatajwa) wameendelea kusema kuwa semi ina tanzu kama vile misemo. Mfano wa usemi walioutoa ni “mtoto wa nyoka ni nyoka” katika mafumbo kuna utanzu wa vitendawili na mizungu. Ufafanuzi wao ulilingana na ule wa TUKI (1990). Mturo

(2011) yeye ameeleza kuwa semi ni kipande cha fasihi simulizi ingawa kwa sasa imo katika fasihi andishi, hii ni kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia kwani inahifadhiwa kwa njia ya maandishi. Ugawanyaji wake haukutofautiana sana na wataalamu wenzake kama Mulokozi (keshatajwa), ila yaye hakukigusia kipera cha lakabu. Madumulla (2005) alieleza kuwa methali ni sentensi za ukweli zinazotokana na ujuzi, sharia, na tabia za jamii ambazo kwa kawaida hushauri hatua za kuchukuwa au kupitisha maamuzi kuhusu jambo au kitendo fulani. Mjadala huu ni muhimu kwa kazi hii, kwa kuwa umemuwezesha mtafiti wa kazi hii kuweza kugunduwa kwa kiasi gani nahau imejitokeza kuwa kama sehemu ya semi na kama zinavyochambuliwa semi nyengine nazo zinahitaji kutafitiwa na kuchambuliwa kwa kina. Hivyo mtafiti wa kazi hii amejikita na kuzichunguza semi.

### 2.2.2 Vipera vya Semi

Vipera vya semi ni methali, vitendawili, nahau na mafumbo. Vipera hivi vimechambuliwa na kufafanuliwa kama inavyoonekana hapo chini.

**Methali**: Methali ni semi fupi zenye mpangilio maalumu wa maneno ambazo huelezwa kwa muhtasari na mafumbo na kuibuwa mawazo mazito yanayotokana na uzoefu wa kijamii, methali huundwa kwa vipande viwili vya maneno vyenye fikra fulani. Kipande cha kwanza huashiria tendo au masharti, na kipande cha pili huashiria matokeo ya tendo au masharti. Mfano “chovya chovya humaliza buyu la asali”. ,”Mcheka kilema hafi hakijamfika” Mehtali huwa na matumizi ya lugha maalumu yanayozipa mvuto kuzifanya zikumbukike. Moja ya haya ni matumizi ya tamathali za semi kama tashbiha, kejeli, msisitizo ukinzani n.k Mfano a) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. b) Leo ni leo asemae kesho muongo. c) Kupotea njia ndio

kujua njia. Mbinu nyengine za kisanaa zinazotumika katika methali ni kama vile takriri, maswali na mchezo wa maneno. Matumizi mengine ya lugha katika methali ni picha au taswira. Picha hizo zaweza kuhusu wadudu, mimea, ndege n.k. Mfano:-

i) Mti mkubwa umeanguka ndege wamashakani.

ii) Ulimi hauna mfupa.

Maana ya methali hutegemea tajriba ya wanaozitumia na miktadha maalumu katika jamii . Kwa hiyo, methali hufanya kazi mbali mbali kama vile kuonya, kushauri, kuhimiza, kukejeli n.k. Mfano.

i) Chema chajiuza kibaya chajitembeza

ii) Mwenda pole hajikwai.

iii) Mkaidi hafaidi mpaka siku ya idi. (R. kaduguda, J. Kiango na Ipara 2015)

**Vitendawili** ; Vitendawili ni aina ya maswali yanayotumia sana lugha ya picha ili kufanya yawe mafupi.Vitendawili hufikirisha na kuwafanya watu wahusishe hali halisi ya maisha na vitu au matukio mbali mbali katika mazingira yao na duniani kwa ujumla. Mfano a) Blangeti la babu lina chawa. (mbingu na nyota) Hapa mbingu imefananishwa na blangeti, wakati nyota zimefananishwa na chawa.b) Kwa mjomba siendi tena. (kuanguka kwa jani) Hapa mtu inabidi afikirie tendo ambalo hutokea mara moja na haliwezi kijirudia. Kwa mfano kuanguka kwa jani, ambako haiwezekani kurejea tena mtini, kumefananishwa na mtu aliyetoka kwa mjomba wake na asirejee huko tena. Vitendawili hutumia luhga ya picha yenye maneno ambayo aghlabu huwa na mpangilio wa kishairi, hutumia tamathali za semi kama sitiari, tash-biha, au tabaini. Mfano “Cha mtaluma mlango wa chuma, ukiufungua

hauna huruma.” Pia hutumia taswira na picha Kwa mfano kamba yangu ndefu haifungi mzigo. Halikadhalika vitendawili hutumia mbinu za kisanaa kama vile tanakali za sauti na takriri. Mfano “Parr!! mpaka maka”. ( R. Kaduguda, J. Kiango na T. Ipara 2015).

**Mafumbo:** Mafumbo ni semi au kauli za maonyo au mawaidha zenye maana iliyofichika. Mafumbo hutolewa kwa kuficha ili kuwakilisha walengwa. Mafumbo hubuniwa kwa shabaha na kwa ajili ya hadhira maalumu. Kauli za mafumbo hutumia lugha ya picha. Mfano “Anijengae hana haja namei, aninunuaye hanitumii, anitumiaye hanioni.” (Jenenza). (R. Kaduguda , J.Kiango na T. Ipara 2015)

**Misemo:** Misemo ni mafungu ya maneno yanayotumiwa na jamii kwa namna maalumu ili kutoa maana inayoafiki ukweli fulani. Misemo hueleza maana ya kauli moja . Misemo hutumia maneno ya kawaida lakini yenye hoja au maana maalumu. Mfano (a) akili ni mali ( b) mtu ni utu (c) kufa kufaana . (R Kaduguda, J.Kiango na T.Ipara 2015).

**Nahau :** Nahau ni kauli fupi fupi zinazotumia sana lugha ya picha. (R. Kaduguda , J . Kiango na T. Ipara 2015) Nahau hutumia maneno ya kawaida lakini hutoa maana tofauti. Unaweza kufahamu maana za maneno yaliyotumika katika nahau, lakini bado ukashindwa kuelewa maana ya nahau hiyo. Aghlabu nahau huundwa kwa kitenzi na nomino. Mfano

i) )Kuwa na mkono mrefu (mwizi)

ii) Mwenye mkono wa birika (bakhili).

iii) Kufunga pingu za maisha (kufunga ndoa)

## 2.3 Dhana ya Maana

Dhana ya maana imejadiliwa na wataalamu mbalimbali miongoni mwa wataalamu hao ni:-TUKI (1990:39) wanasema maana ni fahiwa ya neno au kirai ama dhana, matumizi au kitajwa. Nae Massamba (2004:47-48) anasema maana ni kile ambacho neno au tungo huashiria kutokana na nadharia matumizi au kitajwa. Pia Maana ni tafsiri ya kitu au jambo, maelezo ya kufanya jambo lieleweke wazi wazi. Kwa upande wa Mnata.R(2014:109) anasema maana ni tafsiri anayokuwa nayo msemaji au msikilizaji. Akaendelea kusema kikawaida maana huwezi kuiona bali huwa katika ubongo wa mtu anayeitafsiri maana.

### 2.3.1 Maana katika Mtazamo wa Kisemantiki

Semantiki ni utanzu wa isimu unaochunguza maana katika lugha ya mwanadamu. Semantiki hutafiti maana za fonimu, mofimu, neno na tungo. Mnata anaelaza kuwa Semantiki hujikita katika kueleza maana mbali mbali za maneno hasa maana za msingi iliyomo katika kamusia mbapo mtumiaji wa lugha huelewa kile kilichokusudiwa bila ya kuwa na maana ya ziada. Kwa mfano “sungura” kisemantiki maana yake ni mnyama mdogo mwenye masikio mafupi. Wakati neno “jembe” maana yake ni kifaa kinachotumika kuchimbulia ardhi. Mnata.R (2014).

### 2.3.2 Maana katika Mtazamo wa Kipragmatiki

Pragmatiki ni taaluma ya isimu jamii ambayo huchanganua lugha kwa kutegemea maoni ya mtumiaji hasa uchunguzi wa miundo ya maneno yanayoleta vikwazo vya kijamii anavyokabiliana navyo katika kutumia lugha na athari za kijamii za matumizi ya lugha (matumizi ya lugha kutokana na mazingira au muktadha.TUKI (1990).

Katika pragmatiki maana mbali mbali za maneno huelezwa kulingana na muktadha wa neno au maneno yalivyotumika. Kwa mfano neno "sungura "kipragmatiki linaweza kuwa na maana zifuatazo:- mwoga, laghai, mjanja. Kwa upande mwengine neno "jembe" kipragmatiki lina maana zifuatazo:- Mkali, hodari au mtu asiyekwama katika jambo lolote.

## 2.4 Kazi Tangulizi kuhusu Semi

Kama tulivyokwisha dokeza hapo mwanzoni kuwa semi zimeshafanyiwa uchunguzi ni watu wengi sana miongono mwao ni :-

Mauya (2006) alifanya utafiti unaohusu maandishi katika vazi la kanga wanazovaa wanawake. Mauya alishughulikia migogoro pamoja na dukuduku ambazo akina mama huwa wanazo na kufanyiana wao kwa wao, pamoja na masuala ya wivu na umbea wa wanawake, kufanyiana fitina nakadhalika. Haya yalielezwa kupitia misemo iliyoandikwa kwenye kanga. Utafiti huu umemsaidia mtafiti wa kazi hii kwa kiasi kikubwa kwani kutokana na uchunguzi wa Mauya mtafiti amepata mwanga na kuelewa kuwa haya yote ni maswala ya kiutamaduni mila na desturi za Waswahili ila jambo hilo linaweza kueleweka na jamii au wazawa wa uswahilini tu. Pamoja na hayo mtafiti ameona kuwa uchunguzi wa Mauya ilikuwa ni kuweka bayana baadhi ya mambo kama vile matumizi ya lugha na aliyaangalia mambo hayo katika mtazamo wa kifasihi. Utafiti huu kwa upande mwengine ulilenga kuchunguza jinsi nahau za Kiswahili sanifu zinavyokwamisha mawsiliano kwa wanaojifunza lugha bila shaka katika kufikia shabaha ya utafiti huu uchambuzi wa maana kwa misingi ya kiisimu ulitumika. Pia Alhabib (2012) alifanya utafiti unaohusiana matumizi ya

taswira katika nyimbo za taarab. Matokeo ya utafiti wake aligundua kuwa kipengele cha misemo kinajidhihirisha katika nyimbo za taarab. Sio aghlabu katika nyimbo za taarab kukosa misemo japokatika kiwango kidogo. Hii ni kwa sababu katika semi ndimo munamopatikana uwasilishaji wa dhamira mbali mbali kwa hadhira inayohusika. Utafiti wake una mchango mkubwa katika utafiti huu kwani umeweza kuzibainisha semi zinazojitokeza katika nyanja nyengine kama vile katika nyimbo za taarabu. Na jambo hili limempa mtafiti hamu ya kuangazia kipengele cha nahau ambacho Alhabib hajakigusia katika utafiti wake. Jambo hili limemlazimisha mtafiti wa kazi hii kuangazia mada ya semi kwa kujikita kwenye eneo la nahau na jinsi zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha. Vile vile Rajab (2012) alichunguza dhima za misemo iliyoandikwa katika fulana katika jiji la Dar es salaam mbapo alishughulikia zaidi kipengele cha dhamira na matumizi ya lugha. Katika utafiti wake huo aliogundua kuwa vazi la fulana limejaa dhamira mbali mbali. Alizitaja dhamira hizo kuwa ni umasikini, hali ngumu ya maisha, UKIMWI, dini, elimu, chuki maisha, umuhimu wa kufanya kazi, vita dhidi ya magonjwa. Amesema kwamba dhamira hizo zimekwenda sambamba na mambo yaliyopo katika jamii.

Kwa upamde wa kipengele cha lugha Rajab amegundua kuwa maandishi yaliyomo katika fulana yana matumizi ya lugha kama vile tamathali za semi, majigambo, maneno ya mitaani na misemo. Utafiti wake unatoa mchango kwa kiasi fulani katika utafiti huu kwani inavyoonyesha dhamira hizo ziko katika mafumbo yanayohitaji kufumbuliwa. Hata hivyo mtafiti wa utafiti huu ameona Rajab amewacha mwanya katika utafiti wake huo kwani wanaozisoma fulana hizo sio weledi wa lugha ya

Kiswahili pekee bali na wageni wa lugha hiyo. Utafiti huu umechunguza nahau zinavyokwamisha mawsiliano kwa wageni wa lugha, na kwa kawaida nahau inawasilisha lugha ya uficho inayohitaji kutolewa ufafanuzi ambao mgeni wa lugha hawezi kuufanya, wala hawezi kuelewa maana iliyokusudiwa katika nahau hii bila kupata ufafanuzi kwa mwenyeji wa lugha. Uledi (2012) naye alichunguza muundo wa vipengele vya lugha katika methali na vitendawili kwa jamii ya wamakunduchi kwa kulinganisha semi za kimakunduchi na zile za Kiswahili Sanifu. Aligundua kwamba katika methali na vitendawili kuna vipengele mbali mbali vya lugha vinavyotumika katika ujenzi wake. Utafiti wake unatoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwani utafiti huu utasadia kuonesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyowasilishwa na semi hususan nahau zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha hiyo.

## 2.5 Pengo la Utafiti

Maandiko mengi mbali mbali yaliyoandikwa juu ya mada ya semi za Kiswahili yalijikita katika kuangalia vipengele mbali mbali vya semi katika mtazamo wa kifasihi ambapo maandiko haya yalichambua dhima, ujumbe, na vipengele vyengine vinavyohusiana na fasihi . Hivyo, mtafiti wa kazi hii alikusudia kupunguza mwanya ulioachwa na watafiti wengine kwani lengo lake lilikuwa ni kuchunguza usemi wa kitanzu cha nahau katika kiwango cha semantiki na pragmantiki ambapo kwa jitihada na uelewa wa mtafiti eneo hili limesahauliwa kwa muktadha huu ndio mtafiti wa kazi hii akaamua kwa maksudi kufanya mada inayosema “Kuchunguza jinsi nahau za Kiswahili sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi kwa wageni wa lugha”.

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia

Katika utafiti kazi yoyote ile lazima itumie nadharia ambayo inakubaliana au kushabihiana na kazi hiyo.

### 2.6.1 Maana ya Nadharia

Massamba (2004:63) anasema kwamba nadharia ni kanuni na misingi ambayo hujengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kueleza jambo. Kwa mujibu wa fasili hiyo neno nadharia linamaanisha maelezo ya jambo yaliyofungamana na vigezo vilivyowekwa au vilivyozalishwa kutokana na uchunguzi yakinifu uliofanywa na kuthibitika kwa ushahidi wa kisayansi. Vigezo hivyo ndivyo vinavyounda kanuni na msingi wa kulieleza jambo lililokusudiwa. "Nadhria ni mawazo maelezo au muongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani" (Kamusi la Kiswahili Sanifu 2004:200). Kamusi kamili ya Kiswahili (2009:363) inaeleza kuwa nadharia ni "mpango wa mawazo au muongozo uliotungwa ili kueleza jinsi ya kufanya au kutekelaza jambo fulani". Mushengezi (2003) naye anasema kuwa nadharia ni maarifa yaliyopangwa ili kueleza dhamira fulani au wazo fulani. Nadharia huchukuliwa kuwa ni dira ya kumuongoza mtafiti au mchambuzi kulikabali na kulielezea vyema jambo fulani kwa mtazamo ambao mtafiti ameujengea imani kwamba unaweza kuleta manufaa zaidi kuliko mtazamo mwengine pindi ukitumika. Nadharia hutoa muongozo katika kutatua jambo ambalo halijaweza kuhakikishwa ukweli wake. Hivyo basi kwa mada hii ya "Kuchunguza jinsi Nahau za Kiswahili Sanifu zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lugha". Mtafiti ametumia nadharia za maana ambazo ziko nyingi. Katika kazi hii alitumia nadharia

mbili ambazo ni (i) Nadharia ya Maaana ya Matumizi (ii) Nadharia ya Maana ya Kimuktadha.

### 2.6.2 Nadharia ya Maana ya Matumizi

Muasisi wa nadharia hii ni Ludwing Wittgenstein (1953) na imeelezwa katika kitabu cha Philosophical Investigation (Riemer 2010, Akmajian na wenzake 2010). Wittegnstein (keshatajwa ) anaeleza kuwa ni kosa kubwa kuweka mipaka ya maana kama ambavyo nadharia ya maana kama dhana, mwitiko na kitajwa zinavyofanya, kwani kufanya hivyo ni sawa na kuweka mipaka ya thamani ya umbo lenyewe la kiisimu. Kinachopaswa kuzingatiwa ni matumizi ya nadharia, na kwa kweli nadharia hii inajikita na kusisitiza kuwa maana ya neno katika lugha ni matumizi yake. Hivyo haina haja ya kuuliza neno hili lina maana gani bali angalia vipi neno hilo linavyotumika. Ullman (1967), Lyons(1987); Fodor(1980); Akmajian na wenzake (2010) pamoja na Reimer (2010) kwa upande mwengine wanaeleza kuwa namna bora ya kueleza maana kisayansi ni kuepuka dhana zisizoonekana wala kuthibitika na badala yake tuagnalie uhalisiya, yaanni matumizi ya lugha kwa kuzingatia muktadha. Wittgenstein (keshatajwa) anafafanua zaidi kuwa lugha hufungamanishwa na tabia zetu na namna tunavyohusiana na watu wengine. Tunatumia lugha kutoa amri, kujibu maswali, kusalimiana na kadhalika. Hivyo lugha lazima itazamwe kama kifaa na sio kitu dhahania. Uelewaji wa maana ya umbo lolote lile la kiisimu ni lazima uzingatie namna lugha inavyotumika. Katika kushadidia zaidi juu ya umuhimu wa nadharia hii, Tobing (2010) anaeleza kuwa maana za maneno hazitakuwa na uvulivuli kama zitakitwa katika muktadha matumizi. Akitililia mkazo zaidi juu ya umuhimu wa nadharia hii Fodor (1980) anaeleza kuwa nadharia hii haibagui umbo lolote la

kiisimu lenye maana. Maneno ya Kiswahili kama vile kwa, na, ya, wa hayana kitajwa wala kuashiria dhana fulani akilini, lakini huweza kuelezwa kwa kutumia nadharia hii ya maana kama matumizi. Wijaya na Yeniterzi (2011) wanaeleza kuwa maneno hubadilika kimaana na mabadiliko hayo huakisiwa katika namna au jinsi maneno hayo yanavyotumika katika miktadha tofauti. Kasoro ya nadharia hii ni kwamba kuelewa maana hakuleti uelewa wowote wa neno hadi liwe katika matumizi. Kwa mfano neno “mbuzi” linapata maana kulingana na linapotumika kama ni kifaa cha kukunia nazi au ni aina ya mnyama. Akmajian na wenzake (2010) wameainisha udhaifu wa nadharia hii kuwa haijaweka wazi mipaka ya kimatumizi ni ipi. Pamoja na mapungufu hayo kuteuwa kwa nadharia hii sio kwa kiholela tu bali kwa kuzingatia ubora wake hasa katika kuelezea maana ya nahau kipragmatiki kwamba haitoi maana kwa kuangalia umbo la neno katika mazingira ya kawaida.

### 2.6.3 Nadharia ya Maana Kimuktadha

Waasisi wa nadharia hii ni Wanaisimu ambao wanadai kuwa maana ya neno, dhana au hali fulani kutokana na muktadha uliopo au unaowazunguka watumiji wa lugha. Katika nadharia hii muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufasiri wa maana. Nadharia hii hupinga matumizi ya kamusi katika kufafanua maana kwa msingi kwamba kamusi haibainishi muktadha wa matumizi ya neno husika. Wanaisimu hawa waliainisha aina tatu za muktadha. Muktadha wa kijamii, muktadha wa usemi na muktadha wa kiisimu. Kwa kuzingatia muktadha wa kijamii kuna baadhi ya maneno ambayo huwa na maana katika jamii fulani na yasiwe na maana katika jamii nyingine. Vilevile yapo baadhi ya maneno ambayo yana maana katika mazingira fulani kimuktadha lakini hayana maana katika mazingira hayo hayo katika hali ya

kawaida. Muktadha wa usemi huongoza uteuzi wa matumizi ya maneno mbalimbali. Hivyo matumizi ya kila neno lazima yaendane na muktadha mwafaka. Kwa mfano "chai moja " usemi huu huendana na muktadha wa hotelini. Usemi huu ukitumiwa kwenye nyumba za ibada utazua utata. Sungura alipokuwa porini akaona matunda mtini yameiva, alipoyarukia akashindwa kuyakamata, alisema "sizitaki mbichi hizi" kumbe ni muktadha tu ulimlazimisha kusema hazitaki mbichi hizo, lakini ukweli unabakia pale pale kwamba sungura alitamani sana zile ndizi juu ya mti ( Mnata 2014). Nadharia hii imemsaidia mtafiti wa kazi hii kwa kulichambualengo la tatu hasa katika kubainisha nahau zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha kutokana na namna ya matumizi ya nahau hizo ambazo zaidi zinatafsiriwa kimuktadha.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imeeleza mapitio ya kazi tangulizi ambazo alitalii mtafiti na kumwezesha kupata welewa wa kutosha juu ya jambo alilolifanyia utafiti. Pengo la utafiti. Mwisho sura imemalizia kwa kubainisha na kuzitolea ufafanuzi nadharia ya maana kimuktadha na nadharia ya maana kimatumizi ambazo ndizo zilizomuongoza mtafiti katika utafiti wake, pamoja na hitimisho la sura nzima.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii inahusiana na mpango mzima wa utafiti jinsi ulivyofanywa na mbinu za utafiti zinazohusiana na ukusanyaji pamoja na uchambuzi wa data. Vipengele vilivyobainishwa katika sura hii ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji , data na aina zake, mbinu za kukusanyia na kuchambua data, maadili ya utafiti na mwisho ni muhtasri wa sura nzima

.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo. Katika utafiti huu data zimepangwa, kuchambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Jambo ambalo limemfanya mtafiti kuamua kutumia muundo wa kimaelezo ni kwamba utafiti huu unahusiana na uchambuzi wa maswala ya lugha. Lugha siku zote huelezeka na kuchambuliwa vizuri zaidi kwa maelezo na siyo takwimu na kwa hivyo mtafiti wa kazi hii ameona njia ya maelezo ni ya ufanisi na yenye kufaa zaidi kuliko ile ya kitakwimu. Na hivyo matumizi ya muundo huu yamwezesha kukusanya, kupanga, kuchambua na kuziwasilisha data kwa urahisi na usahihi zaidi kuliko angetumia njia ya kitakwimu.

## 3.3 Kundi Lengwa

Kwa mujibu wa Bryman (2004; Kombo na Trom 2006) Kundi lengwa ni jumla ya watu wote au vitu vyote ambavyo huhusishwa katika utafiti na mtafiti huvitumia katika kupata data zinazohitajika. Kutokana na ukweli kuwa itakuwa ni vigumu kushirikisha watu wote katika mchakato wa utafiti, kwa kawaida kundi lengwa ndilo

litakalomuwezesha mtafiti kuteuwa sampuli ambayo ataitumia kuwakilisha watu wengine katika eneo husika la utafiti. Katika utafiti huu kundi lengwa lilikuwa wageni wa lugha ya kiswahili walimu wa Kiswahili katika shule za secondari, wanafunzi wa sanaa shule za sekondari ya juu , pia wanafunzi wanaosomea mafunzo ya ualimu. Mtafiti wa utafiti huu ameamua kutumia kundi lengwa alilolitaja akiamini kwamba kutokana na kundi hilo atakusanya data za kutosha, za kweli na uhakika kwani ni imani yake kwamba kundi hilo lina uelewa wa kutosha kuhusu data zinazohusu mada aliyoifanyia uchunguzi. Hivyo kupitia kundi hilo amefikia malengo aliyojiwekea kwa wakati muafaka.

## 3.4 Sampuli

Kwa mujibu wa Kothari (2014) Sampuli ni watafitiwa ambao wameteuliwa kutoka katika kundi kubwa ili watumike katika utafiti. Watafitiwa hao huweza kuwa watu au vitu ambavyo mtafiti huteuwa kwa ajili ya kufanyia utafiti wake, kwa kuzikangatia malengo na aina ya utafiti husika. Utafiti huu ulitumia sampuli ya watu 90 wakiwemo wageni wa lugha ya kiswahili 10 wakiwemo wanawake 4 na wamaume 6 wazawa wa lugha wanafunzi 70 ambapo wanafunzi 35 walikuwa ni wakike na wanafunzi 35 wa kiume na walimu walikuwa ni 10 ambapo walimu 5 walikuwa ni wa kiume na walimu 5 ni wa kike.

## 3.5 Usampulishaji

Kwa mujibu wa Suwedi (2013) akimnukuu (Bryman 2004) anaeleza kuwa uteuzi wasampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kutumika katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi

zima. Naye Besti (1996) anasema kuwa usampulishaji ni njia au utaratibu wa kuteuwa washiriki wachache kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa wote. Usampulishaji uko wa aina kadhaa. Utafiti huu umetumia usampulishaji wa mbinu ya malengo maalumu (purposive sampling). Hii ni moja wapo wa mbinu ya kuteulia sampuli ambayo mtafiti huzingatia malengo maalumu wakati wa kuteua sampuli yake. Mtafiti wa utafiti huu ameamua kuteua mbinu hii ya kupata sampuli kutokana na tegemeo kuwa sampuli atakayoichagua kupitia mbinu hii itamwezesha kupata data zake kwa urahisi na uhakika wa hali ya juu na zitakua ni zile data mahsusi anazozihitaji hasa. Jambo ambalo lilikuwa kama aliyotarajia mtafiti.

## 3.6 Maana ya Data

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) Data ni mkusanyiko wa taarifa za kiuchunguzi wa kitaalamu unaopelekea kupatikana usahihi wa jambo. Aidha Advanced Learners Dictionanry (2003) linasema data ni kukisoma kitu kwa undani (kwa makini) na kujaribu kugundua ukweli mpya kuhusu jambo hilo.  Hata hivyo Kamuzore na wenzake (2008) wanasema data ni pale mtafiti anapotafuta taarifa za ukweli kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi.

### 3.6.1 Aina za Data

Utafiti huu utafanywa kwa kutumia aina mbili za data ambazo ni data za msingi na data za upili.

#### 3.6.1.1 Data za Msingi

Kamili (2008) anasema data za msingi ni data ambazo hukusanywa moja kwa moja kutoka eneo la utafiti na mtafiti mwenyewe ambapo hutumia viungo vyake vya hisia

kama vile mdomo, macho, ngozi na pua. Anafafanua zaidi kwa kusema kuwa aina hizi za data huwa ni za ukweli na uhakika na huwa zinaenda na wakati. Pia Kothari (2004) anasema kuwa Data za msingi ni data ambazo mtafiti hukusanya mwenyewe katika eneo la utafiti. Mtafiti wa kazi hii alikusanya data zake za msingi katika maeneo tofauti ambayo ni katika shule ya Utaani, Uweleni na chuo cha ualimu kilichoko Micheweni katika kisiwa cha Pemba.

#### 3.6.1.2 Data za Upili

Kwa mujibu wa Kothari (2004) data za upuli ni data ambazo hupatikana kupitia mapitio ya kazi tangulizi, kama vile magazeti, majarida, vitabu mbali mbali na tafiti za watu wengine. Kamili (2008) anasema hizi ni data ambazo hukusanywa na mtafiti mwenyewe katika vyanzo mbali mbali vya habari kama vile vitabu, magazeti, majarida mbali mbali na kadhalika. Anafafanua zaidi kwa kusema kuwa taarifa hizi huwa tayari zimesha chapwa au tayari zimeshaandaliwa. Ambazo huonekana ndani ya vitabu, majarida ya kielimu, magazeti, tafiti za watu, jumuiya binafsi na wizara za serikali. Mtafiti wa utafiti huu alikukusanya data hizi za upili katika maktaba ya Chake Chake na Wete kisiwani pemba, pamoja na katika mitandao.

## 3.7 Mbinu za Kukusanyia Data

Mbinu za kukusanya data ni njia na zana zinazitumika katika kukusanya taarifa za kiutafiti katika kutolea majumuisho. (Kombo na Tromp, 2006 na Kothari 2008).Wataalamu hawa wamependekeza matumizi ya njia zaidi ya moja ili kupata taarifa zilizo sahihi. Ziko mbinu nyingi za kukusanyia data ambazo ni kama vile dodoso na mahojiano uchunguzi makinina nyingi nyinginezo. Mtafiti wa utafiti huu

alitumia mbinu ya dodoso na mahojiano kwa ajili ya kukusanya data. Mtafiti ameamua kutumia mbinu hizi mbili kutokana na matakwa ya mada husika na kwa imani kwamba mbinu hizi mbili zitamuwezesha kupata data nyingi na za kutosha na ambazo zitaweza kumfikisha safari yake aliyoikusudia bila ya matatizo.

### 3.7.1 Dodoso

Dodoso ni maswali ambayo huandikwa kwenye karatasi na kupewa walengwa mkononi au kupelekwa kwa njia ya barua pepe ambapo walengwa hupaswa kujibu maswali hayo na baadaye kuyarudisha kwa mtafiti (Kamili, 2008). Pia Bukagile na wenzake (2005) wanasema dodoso ni mbinu ya kukusanya data ambayo inahusisha maswali yaliyofungwa na yale yaliyo wazi kwa njia ya maandishi na kupelekwa kwa walengwa ili yajibiwe. Mtafiti ameteua kutumia mbinu hii kwa sababu, mbinu ya dodoso inaweza kutumika hata kama kuna sampuli ndogo katika eneo la utafiti. Pia mbinu ya dodoso inapelekea urahisi wa kuzichambua data kwa vile zinatoa maelezo kidogo. Vilevile mbinu ya dodoso inaonekana kuwa inawavutia watu wengi kwa vile katika ufanyaji wake hakutumiki jina lamtafitiwa. Kwa upande mwengine mbinu hii gharama yake ni ndogo na inaweza kuwafikia watafitiwa wengi kadiri inavyowezekana. Katika kutafiti huu dodoso lilitumiwa kwa wamafunzi kwa sababu niniamini kwamba wakati nikitaka waeleze juu ya jambo fulani maelezo yao hayatokuwa ya kina na ufasahawa kutosha.

### 3.7.2 Mahojiano

Mahojiano ni majadiliano baina ya mtafiti na mtafitiwa. Katika mbinu hii hufanyika mjadala wa ana kwa ana au kwa njia ya simu baina ya mtafiti na mtafitiwa.

(Kamuzore na wenzake 2008). Oxford Dictionary (2003) linasema mahojiano ni majadiliano ya siri baina ya mtu na watu ambapo maswali huulizwa na kujibiwa. Mtafiti wa kazi hii aliamua kuchagua mbinu hii kwa sababu mtafiti anafahamu kuwa mbinu ya mahojiano humpa fursa mtafiti kuweza kujua mengi yaliyojificha kwa watafitiwa.Vile vile njia hii humfanya mtafiti kupata majibu kwa haraka zaidi. Pia mbinu hii ni nzuri kwani inatumika. Kwa wote wanaojua kusoma na wasiojua kusoma, jambo hili humfanya mtafiti kuweza kukusanya data nyingi kuliko alivyotegemea. Pia kupitia mbinu hii mtafiti hupata fursa ya kuweza kujua swali alilouliza kwa mlengwa limefahamika au halikufahamika na kupata fursa ya kutoa ufafanuzi wa ziada pale inapobidi. Katika utafiti huu mbinu hii ya mahojino ilitumika kwa watafitiwa walimu pamoja na wageni wa lugha. Mtafiti aliamua kutumia mbinu hiikwa watafitiwa hawa kwanza kwa upande wa walimu wana uwezo wa kutosha wa kutoa maelezo ya kina , pia walimu wana kiwango kikubwa cha elimu hivyomaelezi yao yanakuwa na umakini wa hali ya juu.Lakini kwaupande wa watafitiwa wageni mtafiti alichelewa watafitwa wake kutoweza kutoa taarifa kwa sababu ya uelewa wao mdogo wa lugha hii ya kiswahili.

### 3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Kwa mujibu wa Jamal na Kamuzora (2008) wakimnukuu Kothari (2004) wanasema uchambuzi wa data ni mchakato wa kuchanganua taarifa Fulani zilizopo ili kupata mpangilio wa mahusiano miongoni mwa makundi mbali mbali ya taarifa zilizokusanywa. Baada ya kuzipata data za utafiti huu matafiti alizichambua data kwa njia ya maelezo na majaduweli, data ambazo zimechambuliwa kwa njia ya majaduweli zimefafanuliwa zaidi kwa kuwekwa maelezo ya kina. Pia mtafiti

ametumia uhakiki wa maelezo katika uchambuzi wa data. Kwa upande wa data zinazohusiana na maana kipragmatiki zimechambuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya maana katika matumizi na nadharia ya maana katika muktadha. Mtafiti ameamua kutumia mbinu zilizotajwa hapo awali kwa vile sehemu kubwa ya utafiti huu imetawaliwa na maelezo, pia kutokana na maumbile ya mada husika. Na Hivyo, mbinu ya maelezo inaonekana kufaa zaidi kuliko mbinu ya kimahesabu ambayo katika utafiti huu haikuweza kuzingatiwa.

### 3.9 Maadili ya utafiti

Madili ni kaida zinazoelekeza tabia zetu katika mahusiano yetu ya kila siku na wenzetu (Matholoko na wenzake ; 2007:15) Katika utafiti maadili ni uwajibikaji na uwelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale tunaotangamana nao katika utafiti, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu (Shaame 2015) Utafiti huu umefanyika katika taasisi mbali mbali za kiserikali na katika serikali kuna sheria na kaununi maalumu za kufuatwa. Hivyo mtafiti alihitaji kuwa na utambulisho maalumu uliweza kumsaidia kuingia katika taasisi hizo bila ya matatizo. Aidha kwa vile jambo hili ni la mtafiti binafsi. Mtafiti alilazimika kuomba ridhaa kwa watafitiwa walikaoshiriki kutoa data. Hii ni kutokana na imani yake kuwa ushiriki wao ni wa hiari. Vile vile wakati wa kutoa muongozo tangulizi juu ya maswali ya dodoso na mahojiano mtafiti aliweka bayana malengo ya utafiti na uzingativu wa suala la usiri na kuahidi kuwa data hizo hazitomuhusu mtu mwengine wala taasisi nyingine zaidi ya mtafiti.

### 3.10 Hitimisho

Sura hii imeksanya vipengele tofauti  kama vile muundo wa utafiti, Kundi lengwa, sampuli na usampulihsaji, data na aina zake, na njia za kukusanyia data, njia za kuchambua data, maadili ya utafiti na kumalizia na hitimisho la sura nzima.

# SURA YA NNE

## 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

### 4.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti unaohusu mada isemayo "Kuchunguza Nahau za Kiswahili jinsi zinavyokwamisha Mawasiliano fanisi kwa wageni wa Lugha. Data za utafiti huu zilikusanywa kupitia vyanzo tofauti vilivyotajwa katika sura iliyotangulia. Katika uchambuzi wa data hizo nadharia ya maana katika matumizi na nadharia ya maana katika muktadha zimetumika. Sura hii pia inaonesha taarifa zilizokusanywa, kutoka kwa walengwa wa sehemu tofauti. Katika utafiti huu data zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kuongozwa na aina mbili za sampuli.Ya kwanza ni ya watafitiwa wageni na ya pili ni ya watafitiwa wazawa wa lugha kwa upande wa sampuli ya watafitiwa wazawa kulikuwa na pande mbili sampuli A na sampuli B Sampuli A ni wanafunzi wa shule ya sakondari ya Uweleni (Mkoa wa Kusini Pemba) na wanafunzi wa ualimu wa chuo cha Kiislamu Pemba (Mkoa wa Kaskazini Pemba ). Sampuli B ni ya walimu wa shule za sekondari ya Uweleni (Mkoa wa Kusini Pemba) na walimu wa shule ya sekondari ya Utaani (Mkoa wa kaskazini Pemba). Jumla ya watafitiwa wote walikuwa ni tisiini (90) ambapo kumi (10) kati yao ni watafitiwa wa kigeni ambao wanne (4) walikuwa wakikena sita wakiume kwa upande wa watafitiwa wazawa walikuwa sabiini (70) kati yao walikuwa ni wanafunzi na kumi (10) ni walimu. Kwa upande wa wanafunzi (35) walikuwa wanawake na (35) walikuwa wanaume. Katika kundi la waalimu mulikuwa wanawake (5) na wanaume (5).

**Jeduweli Na :4.1 Watafitiwawa Kigeni**

| Aina ya Wageni | Wk | Wu | Jumla |
|---|---|---|---|
| Madaktari wa Kichina | 1 | 2 | 3 |
| Madaktari wa Kikorea | 1 | 1 | 2 |
| Madaktariwa Kikyuba | 1 | 2 | 3 |
| Volunteers wa NGOs | 1 | 1 | 2 |

Chanzo:data kutoka katika utafiti huu 2018

**Jeduwali Na.4.2: Watafitiwa Wanafunzi**

| Miaka | Wk | Wu | Jumla |
|---|---|---|---|
| 15 -18 | 16 | 10 | 26 |
| 19 -21 | 16 | 19 | 35 |
| 22 -24 | 3 | 6 | 9 |

Chanzo: data kutoka utafiti huu (2018)

**Jeduwali Na. 4.3: Watafitiwa Walimu**

| Miaka | Wk | Wu | Jumla |
|---|---|---|---|
| 25 -34 | 2 | 1 | 3 |
| 35 -44 | 1 | 3 | 4 |
| 45 -54 | 2 | 1 | 3 |

Chanzo: data kutoka utafiti huu (2018)

Uteuzi huu ulikuwa na lengo kulinganisha matokeo ya watafitiwa kwani mtafiti aliteua shule katika Mikoa yote miwili ya kisiwa cha Pemba Kwa kushirikisha wageni wa lugha ya kiswahili,walimu na wanafuzi, ambapo uchambuzi wa data umezingatia malengo mahsusi ya utafiti huu ambayo yalikuwa ni:-

i) 1 Kubainisha nahau za Kiswahili kulingana na makundi yake.

ii) Kuchambua maana ya nahau kipragmatiki na kwa kuzingatia maumbo ya maneno yaliyounda nahau hizo.

iii) Kubainisha jinsi nahau zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha.

Data zote za utafiti huu zimekusanywa kupitia mbinu ya dodoso, majadiliano. Kwa ujumla sura imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wa sura, sehemu ya pili ni ubainishaji wa nahau za Kiswahili kwa kuzingatia makundi, sehemu ya tatu ni kuchambua maana ya nahau hizo kipragmatiki na kwa kuzingatia maumbo ya maneno na sehemu ya nne ni kubainisha jinsi gani nahau za Kiswahili zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha ya Kiswahili na sehemu ya tano ni hitimisho.

## 4.2 Kubainisha Nahau za Kiswahili kwa Kuzingatia Makundi

Lengo la kwanza la utafiti huu ni kubainisha nahau za Kiswahili kwa kuzingati makundi yake kimuktadha. Ili kukamilisha matakwa ya lengo hili mtafiti alitumia mbinu ya dodoso, mahojiano na . Mtafiti alikusanya taarifa kutoka kwa walengwa kwa ajili ya kupata majibu ya maswali yanayoakisi lengo la kwanza la utafiti huu. Lengo hili lilikuwa na swali moja lenye sehemu mbili (a) na (b) Suala hili lilijibiwa na jumla ya watafitiwa thamanini (80) sawa na asilimia 100 ya watifitiwa wote. Watafitiwa 40 walikuwa ni wanawake na watafitiwa 40 ni wanaume. Watafitiwa waliojibu kwamba “ndio wamewahi kuzisikia taarifa zinazohusu kuwepo kwa nahau za Kiswahili” ni ( 78) sawa na asilimia 97.5 na watafitiwa wawili tu walijibu kwamba “hapana hawajawahi kuzisikia habari yoyote inayohusiana na kuwepo kwa nahau za Kiswahili” ambao ni sawa na asilimia 2.5 ya watafitiwa wote.

**Jeduwali Na. 4.4: Mgawanyiko wa Majibu ya Watafitiwa**

| Sampuli ya watafitiwa | W ke | Wu | Ndiyo | | Hapana | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Jumla | Asilimia | Jumla | Asilimia |
| SAMPULI A | 35 | 35 | 68 | 85 | 2 | 2.5 |
| SAMPULI B | 5 | 5 | 10 | 12.5 | 0 | 0 |
| JUMLA | 40 | 40 | 78 | 97.5 | 2 | 2.5 |

Chanzo: Data kutoka utafiti huu (2018)

### 4.2.1 Tafsiri ya Matokeo

Jumla ya watafitiwa sitini na wanane (68 ) sawa na asilimia 85 katika sampuli A na watafitiwa kumi (10) sawa na (12.5) kutoka katika sampuli B walishiriki katika kujaza dodoso na kuhojiwa. Jibu lao lilikuwa ni ndio wamewahi kuzisikia nahau za Kiswahili na hivyo waliweza kuzitaja. Kwa muktadha huo Jumla ya watafitiwa sabiini na wanane (78) kutoka sampuli A na B ambao ni sawa na asilimia 97.5 ya watafitiwa wote walijibu ndiyo. Na watafitiwa 2 sawa na asilimia 2.5 ya watafitiwa wote walijibu hapana. Walichokusudia kuonesha ni kuwa hawajawahi kusikia habari inayohusu nahau za Kiswahili na hivyo walishindwa kuzitaja. Hivyo basi, Kutokana na matokeo hayo inaonesha kuwa watu wengi wamewahi kuzisikia nahau za Kiswahili na wanazielewa kwa kiasi kikubwa. Mtafiti amekuja na madai hayo kwa kuwa watafitiwa walio wengi wameweza kuzibainisha nahau za Kiswahili. Zifuatazo ni nahau ambazo zimebainishwa kwa mujibu wa makundi yaokimuktadha kama yanavyoonyeshwa katika jeduwali lifuatalo:-

**Jeduwali Na 4.5: Makundi ya Nahau Zilizobaininishwa**

| s/n | **Idadi** | **Kundi la nahau** |
|---|---|---|
| 1 | 29 | Zinazohusu mila na desturi za jamii |
| 2 | 14 | Zinazohusu juhudi katika kazi |
| 3 | 10 | Zinazohusu choyo na usaliti |
| 4 | 9 | Zenye uhusiano wa dini na imani |
| 5 | 9 | Zinazohusu subira na uvumilivu |
| 6 | 6 | Zinazohusu mambo ya maadili |
| 7 | 3 | Zinazohusu Ushirikiano |
| 8 | 2 | Zinazohusu elimu |

Chanzo: data kutoka utafiti huu (2018**)**

Nahau zilizotajwa na watafititiwa mtafiti aliweza kuzibainisha kwa kuzigawa katika makundi manane (8). Makundi aliyojataja ni pamoja na kundi la nahau zinazohusu mila na desturi za jamii, kundi la nahau zinazohusu juhudi katika kazi, kundi la nahau zinazohusu choyo na usaliti, kundi la nahau zinazohusu dini na imani kundi la nahau zinazohusu subira na uvumilivu, kundi la nahau zinazohusu mambo ya maadili, kundi la nahau zinazohusu ushirikiano na kundi la mwisho ni la nahau zinazohusu elimu.

### 4.2.2 Nahau zinazohusu Mila na Desturi za Jamii

1. Amevunja ungo
2. Anapiga domo
3. Amekula chumvi nyingi
4. Ana mkono mkono
5. Kupigwa kipapai
6. Piga vijembe
7. Kuchimba dawa

8. Kunja uso
9. Kumbatia rufani
10. Kuchungulia kaburi
11. Amevunja chupa
12. Ameaga dunia
13. Lisha nyama ya ulimi
14. Amekula miguu ya kuku
15. Bao la mkahawani
16. Amepiga ndoo teke
17. Kukanyaga nyaya
18. Kuzunguka mbuyu
19. 19Ana jicho la nje
20. Mja mzito
21. Ana mkia wa mbuzi
22. Amelala chali
23. Kunja jamvi
24. Amejifungua
25. Mama huruma
26. Kumkalia mtu kitako
27. Ana kijicho
28. Kunja virago
29. Amefurutuada

### 4.2.3 Nahau Zinazohusu Juhudi katika Kazi

1. Amevuta kamba
2. Amemwaga unga
3. Pita njia ya panya
4. Kenda kombo
5. Ana miguu mirefu
6. Ameukata
7. Ana mkono mrefu
8. Kaza kamba
9. Kupiga mbizi
10. Kaza buti
11. Chapua mguu
12. Amekufa kikondoo
13. Amekula debe
14. Kutia for a

### 4.2.4 Nahau zenye Uhusiano wa Dini na Imani

1. Amemlanda baba yake
2. Kutapikia sandani
3. Mkono mfupi
4. Ana mkono wa buli
5. Ana kichwa kikubwa
6. Ameacha njia
7. Ana roho ya korosho

8. Ana mguu mzito
9. Amekula kichwa cha samaki

### 4.2.5 Nahau Zimazohusu Choyo na Usaliti

1. 1 Kuchomea utambi
2. Ana ndimi mbili
3. Joka la mdimu
4. Amekuwa popo
5. Kupigwa kibuti
6. Kunawa mikono
7. Kukata shingo
8. Kata shauri
9. Kula mlungura
10. Kupaka mafuta kwa nyuma ya chupa

### 4.2.6 Nahau Zinazohusu Subira na Uvumilivu

1. Kujikaza kisabuni
2. Ona cha mtema kuni
3. Mezea mate
4. Kufa na tai shingoni
5. Kuanguka mtungi
6. Kupiga moyo konde
7. Kata maini
8. Kufa moyo

9. kujipalia makaa

### 4.2.7 Nahau Zinazohusiana na Mambo ya Maadili

1. 1Ameasi ukapera
2. Yuko msalani
3. Amepata jiko
4. Amepata ua
5. Kachonga mwiko
6. Andika meza

### 4.2.8 Nahau Zinazohusu Ushirikiano

1. Kushika usukani
2. Jamvi la wageni
3. Aliniunga mkono

### 4.2.9 Nahau Zinazohusu Elimu

**1.** Kuchanganya mawazo
2. Kushika kitabu

## 4.3 Kuchambua Maana ya Nahau Kipragmatiki na kwa Kuzingatia Viambajengo vilivyounda Nahau hizo

Lengo la pilli la utafiti huu lilikuwa ni kchambua maana ya nahau kipragmatiki na kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau hizo. Lengo hili lilijibu swali linalosema kuwa ni zipi maana za kipragmatiki na ni zipi maana za nahau kwa

kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau hizo? Hivyo katika sehemu hii mtafiti ameweza kuzibainisha nahau katika kipengele cha kipragmatiki. Kipengele hiki ni ambapo ni kile chenye kutoa maana ya uficho ambayo sio rahisi mtu kuweza kuelewa. Maana hiyo inakuwa ngumu kuitambua kwa kuwa, ndani ya nahau hizo kunakuwa hakuna dalili za wazi zinazoonesha uwepo wa maana hizo. Kwa muktadha huo ujuzi wa maana za kipragmatiki unahitaji upeo wa juu wa ujuzi wa lugha na utamaduni wa Kiswahili. Katika kutoa maana hizi mtafiti aliongozwa na Nadharia ya maana kimatumizi na nadharia ya maana kimuktadha kama alivyosema Ullman (1967), Lyons (1987); Fodor (1980); Akmajian na wenzake (2010) pamoja na Reimer (2010). Wataalamu hao wameona kuwa namna bora ya kueleza maana kisayansi ni kuepuka dhana zisizoonekana wala kuthibitika na badala yake tuangalie uhalisia, yaani matumizi ya lugha kwa kuzingatia muktadha. Wittgenstein (1953) anafafanua zaidi kuwa lugha hufungamanishwa na tabia zetu na namna tunavyohusiana na watu wengine. Tunatumia lugha kutoa amri, kujibu maswali, kusalimiana na kadhalika. Hivyo lugha lazima itazamwe kama kifaa na sio kitu dhahania. Uelewaji wa maana ya umbo lolote lile la kiisimu ni lazima uzingatie namna lugha inavyotumika. Katika kushadidia zaidi juu ya umuhimu wa nadharia hii, Tobing (2010) anaeleza kuwa maana za maneno hazitakuwa na uvulivuli kama zitakitwa katika muktadha wa matumizi. Hivyo kutokana na maelezo ya wataalamu hawa ndipo matafiti akatumia nadharia ya maana katika matumizi na nadharia ya maana katika muktadha ili zimuongoze katika uchambuzi wa maana za nahau kipragmatiki. Uchambuzi wa nahau hizo unaoneshwa katika jeduwali hapo chini. Kwanza mtafiti ameanza na kuchambua maana za kipragmatiki ikifuatiwa na uchambuzi wa maana za nahau kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau.

Katuka kuchambua maana hizi mtafiti alichagua nahau hamsini (50) katika kila kundi (kundi la nahau zilizotolewa maana ya kipragmatiki na kundi la nahauzilizotolewa maana kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau ). Nahau nyengine zimewasilishwa katika kiambatanisho.

### 4.3.1 Kuchambua Maana ya Nahau Kipragmatiki

**Jeduweli Na 4.6: Maana ya Nahau Kipragmatiki**

| S/Na | **Nahau** | **Maana ya Nahau Kipragmatiki** |
|---|---|---|
| 1 | Ana ndimi mbili | Hana msimamo (mnafiki) |
| 2 | Joka la mdimu | Mtu asiye na haja na kitu lakini anawazuia wenzake wasifaidike na kitu hicho |
| 3 | Kuanguka mtungi | Hali ya mwanamme kupoteza nguvu za kiume |
| 4 | Kuchimba dawa | Kujisaidia haja ndogo au kubwa hasa katika mazingira ya vichakani au maporini. |
| 5 | Ameukata | Amefanikiwa kimaisha |
| 6 | Bao la mkahawani | Kila mtu ni wake hachagui (mwanamke au mwanamme Malaya) |
| 7 | Mkono wazi | Mkarimu |
| 8 | Amekula kichwa cha samaki | Mtu mwenye uzito wa kufahamu |
| 9 | Amepata ua | Amepata mwanamke mzuri |
| 10 | Kukanyaga nyaya | Kupata ukimwi |
| 11 | Amepiga mbizi | Amefanikiwa kimaisha |
| 12 | Kupaka mafuta kwa nyuma ya chupa | Kudanganya (kukejeli) |
| 13 | Kuzunguka mbuyu | Kutoa rushwa |
| 14 | Ana mkono mrefu | Mtu mwenye uwezo wa kupata kitu popote hata kama kiko mbali |
| 15 | Kaza buti | Ongeza juhudi |
| 16 | Mja mzito | Mwanamke mwenye mimba |
| 17 | Ana kichwa kikubwa | Ana akili nyingi |
| 18 | Ana jicho la nje | Muhuni anaependa mwanamke huyu na yule |
| 19 | Amekuwa popo | Hana msimamo |
| 20 | Kupiga moyo konde | Kijitolea muhanga (kuvumilia) |
| 21 | Kata maini | Umia moyoni |
| 22 | Ameasi ukapera | Ameoa |
| 23 | Amevuta kamba | Amefariki |
| 24 | Ana mkono wa buli | Mtu aliyekuwa chake hakipatikani (mbakhili) |
| 25 | Kupigwa kipapai | Kufanyiwa ushirikina (kulogwa ) |
| 26 | Kachanganya mawazo | Hakufahamu |
| 27 | Kupigwa fyagio la chuma | Kufukuzwa kazi |
| 28 | Kula mlugura | Kula rushwa |

| | | |
|---|---|---|
| 29 | Ana mkono mkono | Mwizi |
| 30 | Kaza kamba | Ongeza bidii |
| 31 | Kenda kombo | Kenda kinyume/kakosea |
| 32 | Kuchungulia kaburi | Kuumwa sana (mahtati) |
| 33 | Kuchomea utambi | Kujenga ushawishi kwa ajili ya kumfitinisha mtu |
| 34 | Kujikaza kisabuni | Kufanya jambo huku ukiwa unaumia |
| 35 | Amevunja chupa | Mjamzito aliyeonyesha dalili za kuwa si muda mrefu<br>atajifungua ( kutokwa na maji ya uzazi ) |
| 36 | Ameaga dunia | Amefariki |
| 37 | Piga maji | Kulewa |
| 38 | Kushika usukani | Kuongoza hasa katika mashindano |
| 39 | Kujipalia makaa | Kujitia matatizoni |
| 40 | Ona cha mtema kuni | Pata adhabu kali (usumbufu) |
| 41 | Lisha nyama ya ulimi | Tumia lugha tamu katika kushawishi jambo |
| 42 | Kufa na tai shingoni | Kukwepa aibu |
| 43 | Kufa moyo | Kukata tamaa |
| 44 | Kata maini | Umiza sana |
| 45 | Amewacha njia | Amepotea |
| 46 | Mama huruma | Mwanamke kahaba /Malaya |
| 47 | Kupigwa kibuti | Kukataliwa na mpenzi wako |
| 48 | Aliniunga mkono | Alikubaliana na mimi |
| 49 | Amevunja ungo | Kitendo cha kutoka damu ya hedhi kwa mara ya kwanza na kwa hivyo kubadilika kutoka hatua ya utoto na kuingia utu uzima |
| 50 | Amepata jiko | Ameoa |

Chanzo: Data kutoka nkatika utafiti huu (2018**)**

Katika Kiswahili kuna nahau ambazo ziko katika kiwango cha neno na kiwango cha kirai. Haya yamedhihirika wazi kupitia nahau zilizoorodheshwa na watafitiwa wa utafiti huu. Hayo yamebainishwa na mtafiti wa kazi hii kwenye jeduweli namba 6 na namba 7 hapo chini.

**Jeduweli Na. 4.7: Mfano wa Nahau Katika Kiwango Cha Neno**

| S/N | **Nahau** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1 | Ameukata | Amefanikiwa kimaisha |
| 2 | Amejifungua | Amezaa |

Chanzo: Data kutoka katika utafiti huu (2018)

**Jeduweli Na. 4.8: Mfano wa Nahau Katika Kiwango Cha Kirai**

| S/N | **Nahau** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1 | Ana mkono wa buli | Mbakhili |
| 2 | Aliniunga mkono | Alikubaliana na mimi |
| 3 | Kuaka mafuta kwa nyuma ya chupa | Kudanganya (kukejeli) |
| 4 | Amepata jiko | Ameoa |
| 5 | Amekula chumvi | Ameishi miaka mingi |
| 6 | Mja mzito | Mwanamke mwenye mimba |
| 7 | Kupigwa kibuti | Kukataliwa na mpenzi wako |

Chanzo: Data kutoka katika utafiti huu (2018)

### 4.3.2 Tafsiri ya matokeo

Katika mifano hiyo iliyoonekana katika majeduweli namba 6 na 7 mtafiti amegundu kuwa nahau za Kiswahili zinaweza kuonekana katika viwango tofauti kama vile kiwango cha neno na kiwango cha kirai. Hata hivyo sio kila neno linaweza kuwa ni nahau bali maneno yanayotumika kama nahau yanakuwa na usanii wa aina fulani, halikadhalika na kirai kinachotumika kama nahau kinakuwa na mjengeko maalum wa kisanii. Usanii huu unategemea neno au kirai katika matumizi na muktadha wa matumizi hayo. Mfano wa nahau katika kiwango cha neno ni:_

**N: Ameukata**

**T: Amefanikiwa kimaisha**

**N: Amejifungua**

**T: Amezaa**

Katika mfano huu nahau **ameukata** inaonekana imeundwa kwa neno moja ambalo linatoka katika kategoria ya kitenzi katika wakati timilifu. Neno hili maana yake ni kugawa kitu kizima katika vipande, ila kwa maana ya nahau kama inavyotumika katika Kiswahili ni kufanikiwa kimaisha. kwa hivyo ikiangaliwa maana ya nahau

kama inavyotumika katika kiswahili inaonekana inatoa ujumbe mzito ambao hauwezi kueleweka na watu wanaoielewa lugha ya Kiswahili kijuu juu tu.Vile vile kwa nahau **amejifungua** imejengwa na neno moja ambalo liko katika kategoria ya kitenzi lenye maana ya kuepukana na kuzuizi fulani alichokuwa amefungika nacho, lakini kwa maana ya nahau kama inavyotumika katika Kiswahili ni **kuzaa.** Hivyo basi tunaweza kusema kuwa nahau zinatumika kwa namna ambayo huwezi kuzielewa ila uwe na kiwango kikubwa cha ufahamu wa lugha. Aidha matokeo ya utafiti yanaonesha pia kuwa nahau zinazowakilishwa na neno moja mara nyingi huwa katika kategoria ya kitenzi kama inavyoonesha mifano iliyotangulia.

**Mfano wa nahau katika kiwango cha Kirai**

**N: Ana mkono wa buli**

**T: Mbakhili**

**N: Ameasi ukapera**

**T: Ameoa**

### 4.3.3 Kuchambua Maana za Nahau kwa Kuzingatia Viambajengo vilivyounda Nahau

Katika kipengele hiki maana za nahau zimetolewa kwa kuzingatia maumbo ya maneno yaliyounda nahau hizo. Maana hizi ni zile maana za msingi ambazo zinachunguzwa na kuangalia maumbo ya maneno jinsi yalivyotumika katika vifungu ya manaeno. Katika kutoa maana hizi mtafiti aliongozwa na nadharia ya maana katika matumizi kama alivyobainisha hapo awali. Wittegnstein (1953) anaeleza kuwa ni kosa kubwa kuweka mipaka ya maana kama ambavyo nadharia ya maana kama dhana, mwitiko na kitajwa zinavyofanya, kwani kufanya hivyo ni sawa na

kuweka mipaka ya thamani ya umbo lenyewe la kiisimu. Kinachopaswa kuzingatiwa ni matumizi ya nadharia, na kwa kweli nadharia hii inajikita na kusisitiza kuwa maana ya neno katika lugha ni matumizi yake. Maana ya nahau kwa kuzingatia viambajengo yanafafanuliwa katika jeduwali lifuatalo

**Jeduwali Na 4.9: Maana ya Nahau Kwa Kuzingatia Viambajengo Vilivyounda Nahau**

| s/n | Nahau | Maana ya nahau kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau |
|---|---|---|
| 1 | Ana ndimi mbili | Ana viungo viwili vinavyoitwa ulimi |
| 2 | Joka la mdimu | Nyoka mkubwa anayekaa chini ya mdimu |
| 3 | Kutapikia sandani | Kuchafua nguo inachotumika kuvishia maiti wakati wa kumuandaa kwa ajili ya mazishi |
| 4 | Kuchimba dawa | Kufukua ardhi ili kupata mzizi wa mti ambao unatumika kwa ajili ya matibabu |
| 5 | Ameukata | Amegawa sehemu ndogo ndogo kitu ambacho kilikuwa kizima |
| 6 | Amepiga ndoo teke | Amepindua chombo kinachotumika kutekea au kuwekea maji |
| 7 | Kushika kitabu | Kukamata kitabu |
| 8 | Amejifungua | Ameepukana na kizuizi fulani |
| 9 | Kachonga mwiko | Katengeneza kifaa cha mbao ambacho kinatumika kukorogea chakula wakati wa kupika |
| 10 | Anapiga domo | Kitendo cha kugonga kiungo cha kiumbe kinachoyumika kuzungumzia lugha |
| 11 | Kata maini | Tenganisha kiungo cha kiumbe kinachoitwa ini kutoka mwilini |
| 12 | Amekufa kikondoo | Amekufa kama anavyokufa mnyama anaeitwa kondoo |
| 13 | Kunawa mikono | Kusafisha mikono kwa kutumia maji |
| 14 | Ana kijicho | Ana kiungo cha mwili ambacho kinatumika kwa kuonea ambacho ni kidogo kuliko kawaida |
| 15 | Amekula debe | Ameingiza mkebe tumboni kama anavyoingiza chakula |
| 17 | Kata shauri | Kupinga mawazo yaliyotolewa na wengine |
| 18 | Ameasi ukapera | Kwenda kinyume na taratibu za kijane |
| 19 | Amevuta kamba | Amefanya kitendo cha cha kuvuta kifaa kinachotumika kwa kufungia kitu |
| 20 | Amevunja ungo | Ameharibu kifaa kinachotumika kupepetea nafaka |
| 21 | Amepata jiko | Amemiliki kifaa au sehemu ya kupikia |
| 22 | Amekula chumvi nyingi | Amekula kitu kinachotengenezwa kwa maji ya bahari kinachotumika kuchapuzia chakula |
| 23 | Amemwaga unga | Amedndosha kitu kilicho katika hali ya chembe chembe ndogo sana mfano wa vumbi |
| 24 | Kupigwa kipapai | Kutumwa tunda linaloitwa papai kama kifaa cha kupigia (bakora) |
| 25 | Kachanganya mawazo | Kukusanya fikra za watu tofauti |

| | | |
|---|---|---|
| 26 | Kupigwa fyagio la chuma | Kupigwa kwa kutumia kifaa cha kufyagilia kilichotengenezwa kwa chuma |
| 27 | Kula mlungura | Kula kitu kilichotengenezwa kwa mbao kilicho mfano wa ngoma |
| 28 | Kaza kamba | Kitendo cha kuzidisha kamba iwe imara katika sehemu ilipofungwa |
| 29 | Piga vijembe | Kitendo cha kugonga gona vijembe |
| 30 | Amelala chali | Amelala hali ya kuelekeza tumbo juu |
| 31 | Kakunja uso | Amefinya sehemu ya mbele ya kichwa |
| 32 | Kumbatia rufani | Kushikilia kitu kinachoitwa rufani kwa kutumia mikono pamoja na sehemu yote ya mbele ya mwili |
| 33 | Kenda kombo | Katembea mtu anayeitwa kombo |
| 34 | Kuchungulia kaburi | Kitendo cha kuangalia shimo linalotarajiwa kuingizwa mwili wa kiumbe aliyefariki |
| 35 | Ana mguu mzito | Ana mguu wenye uzito usio wa kawaida |
| 36 | Kuchomea utambi | Kuwasha moto utambi kwa niaba ya mtu |
| 37 | Kujikaza kisabuni | Kustahamili bila uwezo mfano wa sabuni |
| 38 | Amevunja chupa | Amebomoa kifaa kinachotunika kuwekea vitu vyenye hali ya kimiminika |
| 39 | Ameaga dunia | Kitendo cha kutolea dunia mkono wa mwisho |
| 40 | Piga maji | Kitendo cha kuyagonga maji ama kwa mkono au kwa kutumia kitu chochote |
| 41 | Kushika usukani | Kukamata kifaa cha chombo cha usafiri kitachotumika kuelekezea chombo kiende upande fulani |
| 42 | Mezea mate | Kusukuma mate yaende tumboni kwa niba ya mtu au mbele ya mtu |
| 43 | Yuko msalani | Yuko katika kifaa kinachotumika kwa kuswalia |
| 44 | Andika meza | Tumia meza kama kifaa cha kuandikia kwa mfano buku au ubao |
| 45 | Kujipalia makaa | Kutoa vipande vya kuni vilivyochomwa moto kwa ajili yako au ukaviweka karibu yako |
| 46 | Pita njia za panya | Kitendo cha kupita katika sehemu wanazotumia kupita panya |
| 47 | Ona cha mtema kuni | Angalia kitu cha mtu mwenye kazi ya kukata miti kwa ajili ya kupikia |
| 48 | Lisha nyama ya ulimi | Mtilie mtu mdomoni kipande cha ulimi wa mnyama au binaadamu |
| 49 | Amemlanda babae | Kapita juu ya nmwili wa baba yake |
| 50 | Kuanguka mutungi | Kudondoka juu ya chombo ambacho zamani kikitumika kuwekea maji ili yawe baridi |

## 4.4 Kubainisha jinsi Nahau zinavyokwamisha Mawasiliano kwa Wageni wa Lugha ya Kiswahili

Lengo la tatu la utafiti huu ni kubainisha jinsi nahau za Kiswahili zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha. Katika sehemu hii mtafiti amechagua baadhi ya nahau ili kuonesha ni jinsi gani nahau za Kiswahili zinavyosababisha ugumu wa

mawasiliano kwa wageni wa luhga. Mtafiti ametoa mifano kadhaa ya nahau za Kiswahili kama ifuatavyo.

### 4.4.1 Nahau " Amevunja Chupa" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili

Kwa kuangalia vijenzi vyake, nahau hii ina maana kwamba "***kuna mtu ameharibu chombo ambacho kinatumika kuhifadhia vitu vilivyo katika hali ya kimiminika".*** Vimiminika hivyo vinaweza kuwa maji, uji, maziwa na vingine vya mfano wake. Hata hivyo katika Kiswahili nahau hii hutumika katika muktadha wa kuwepo mtu ambae ni mja mzito na tayari ameonesha dalili ya mwisho ya kuwa si muda mrefu atajifungua (kitendo cha kumwagika kwa maji ya uzazi). Muktadha huu unamfanya mgeni wa lugha asiweze kuelewa kusudio la nahau hii. Yeye anachokielewa ni kwamba **"*chupa"*** ni kifaa fulani na ***"kuvunja*"** ni ***kitendo cha kuharibu kitu na kukitoa katika umbo lake na hivyo kutoweza kutumika tena***. Hivyo basi wakati wa utumiwaji wa nahau hii mgeni wa lugha anaweza kushangaa, kujihadhari au kuuliza maswali mfano haikumkata? Au ilikuwaje? Anaweza kuuliza hivyo kwa kuwa yeye katika kumbu kumbu zake chupa ikivunjika inaweza kusababisha madhara kwa aliye karibu nayo. Magae yanaweza kutawanyika na kumsababishia madhara aliyekaribu nayo na pengine hata mvunjaji chupa mwenyewe. Muktadha wa msemaji, mweledi wa lugha na muktadha wa msikilizaji mgeni wa lugha unaonekana wazi kuweka kizingiti cha kimawasiliano baina ya watumiaji wawili hawa. Katika jamii ya Waswahili na katika muktadha wa afya ya uzazi ***kuvunja chupa*** kuna maana ya kufunguka njia ya uzazi na kuanza kutoka maji kuonesha utayari wa kujifungua. Katika matumizi ya lugha na muktadha wa kinahau neno ***kuvunja chupa*** linabeba

maana hii na siyo maana inayoweza kuelezwa vijenzi vya kirai wenyewe. Hii inaonesha wazi jinsi nadharia ya maana kimatumizi na ile ya maana kimuktadha inavyoweze kuwa faafu katika uchambuzi wa nahau hii.

### 4.4.2 Nahau "Kuchimba Dawa" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili

Katika Kiswahili nahau hii ina maana ya ***kujisaidia*** (kwenda haja) katika eneo la kichaka au pori. Lakini maana ya nahau hii kwa kuzingatia viambajenngo vilivyounda nahau maana yake ingekuwa hiki ni kitendo cha ***kufukua ardhi kwa ajili ya kuchimba mzizi wa mti ili kuutumia kwa ajili ya matibabu.*** Matumizi ya nahau hii mbele ya mgeni wa lugha inaweza kupelekea ukosefu wa mawasiliano fanisi. Hili linaweza kujitokeza pale mgeni anapotaka kushiriki katika kufanya kitendo hicho cha kufukua ardhi ili kupata kitu kinachotumika kwa ajili ya matibabu. Inawezekana kuwa mgeni na yeye anasumbuliwa na maradhi fulani hivyo tegemeo lake dawa zinazochimbwa zinaweza kufaa kuwa ni tiba ya maradhi yanayomsumbua. Lakini kwa bahati mbaya mazungumzo haya yalikuwa na lengo la kueleza tendo la kwenda haja msituni na siyo kuchimba dawa. Kwa muktadha huuinaonekana kwamba matumizi ya nahau yanawafanya wageni wa lugha kutoelewa kusudio hasa la nahau iliyozungumzwa. Kwa hakika kirai ***kuchimba dawa*** hakina uhusiano hata mdogo na tafsri yake. ***Kuchimba*** ni kutifua ardhi na ***dawa*** ni kitu kifaacho kwa ajili ya tiba. Lakini maneno haya yamekuwa na maana ya "kujisaidia msituni". Hapa maana hii ni ya kimatumizi na kimuktadha tu. Ni maana inayotolewa kwa mujibu wa muktadha wa kinahau kama inavyoeleweka katika utamaduni wa Waswahili. Hili

linaakisi kabisa nadhari ya maana kimuktdha katika aina yake ya muktadha wa mazingira ya kijamii.

### 4.4.3 Nahau "Amepata jiko" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili

Nahau hii maana yake katika Kiswalihili ni ***kuoa.*** Lakini kwa maana inayoweza kupatikana kwa kuzingatia vijenzi vilivyounda nahau hii tutakuta kwamba maana yake ingeweza kuwa ***amemiliki kifaa cha au sehemu inayotumika kwa kupikia***. Katika matumizi ya nahau kama hii, kwa mfano, kwa hali ya kawaida mtu asiyekuwa mjuzi wa lugha na asiyekuwa mtambuzi wa utamaduni wa Mswahili ataielewa maana ile itokanayo na viambajengo vilivyunda nahau hiyo. Ataelewa hivyo kwa sababu ujuzi wake wa Kiswahili ni wa kuelewa maana za wazi tu. Mara nyingi maana anayoelewa yeye ni ile maana ya kikamusi na kwa hivyo anaweza kujenga picha ya jiko kama kifaa cha kupikia au sehemu ya kupikia. Maana hiyo katika muktadha huu sio sahihi kwani maana iliyokusudiwa hapa imejificha na sio rahisi kuielewa mpaka mtu awe mweledi wa lugha ya Kiswahili na mtambuzi wa utamaduni wa Mswahili. Kwa hivyo nahau amepata jiko ina maana ameoa na sio amemiliki mahali au kifaa cha kupikia. Nadharia mbili tulizozitumia zinatuhimiza kwamba maana katika lugha hujitokeza kimatumizi na kimuktadha na siyo kuangalia maana ya neno moja moja. Kwa hivyo nadharia ya maana kimuktadha kupitia muktadha wa mazingira ya nahau za Kiswahili na muktadha wa jamii ya Waswahili maana itakuwa "***kuoa"*** na siyo kumiliki kifaa kiitwacho jiko au kupata mahali au sehemu ya kupikia.

### 4.4.4 Nahau "Jamvi la Wageni" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Kwa kawaida "jamvi" ni neno linalorejelea ***kifaa kinachotumika kwa kukalia aghalabu kitengenezwacho kwa miyaa au vidaka vichanga vya mvumo.*** Wageni ni ***watu ambao sio wenyeji wa familia fulani au wa pahala fulani.*** Kwa muktadha huo kwa kuangalia maneno yaliyotumika kujenga nahau hii tunaweza kusema maana yake ni ***kifaa kinachotumika kukalia wageni***. Lakini kwa kuzingatia maana ya nahau hii kama inavyotumika katika Kiswahili ni ***mtu ambaye yupo kwa ajili ya wageni. Mtu huyu anakuwa na mazoea na watu wanaokuja ambao hushirikiana, husaidiana nao na huwaelekeza na kuwajuilisha mambo wasiyoyaelewa katika sehemu ile ikiwemo mila na utamaduni, na kuzoeana nao hata kama hawakumjia yeye.*** Hii hasa ndiyo maana yake kimuktadha na kimatumizi katika kipera cha nahau za Kiswahili. Lakini mgeni wa lugha asiyetambua matumizi ya lugha kimuktadha katika uwanja huu wa nahau kama inavyoakisiwa na nadharia zetu teule, anaposikia nahau kama hii anaweza kuelewa kuwa jamvi la wageni ni kifaa cha kukalia kitako na si mtu wa aina fulani. Tofauti hizi za ufahamu kati ya maana ya muktadha na maana inayotokana na vijenzi vya nahau zinaweza kuleta ukinzani wa kimawasiliano kati ya mwenjeji na mgeni wa lugha.

### 4.4.5 Nahau "Amepata Ua" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Maana ya nahau hii kwa kuangalia viambajengo vilivyoiunda ni kuwa ***kuna mtu ambaye amemiliki kiungo cha uzazi cha mti.*** Lakini katika Kiswahili nahau hii ina maana ya kuwa ***amepata mwanamke mzuri. Hivyo ndivyo maana yake ilivyoibuka***

***kimuktadha wa kimatumizi kama inavyoakisiwa na nadharia zetu teule.*** Kwa kuzingatia ruwaza hizi mbili za neno mawasiliano baina ya mzawa wa lugha na mgeni wa lugha yanaweza kukwama. Hii ni kwa sababu mgeni wa lugha hawezi kujua maana hii hasa ya nahau ***inayotumika*** katika Kiswahili. Jambo hili litamsababisha yeye moja kwa moja kutoa tafsiri isiyo sahihi kwani yeye anachoangalia ni maumbo gani ambayo yameunda hiyo nahau na kuyatolea maana yake ya moja kwa moja. Hapo pia patakosekana mawasiliano fanisi kati ya mgeni na mwenyeji wa lugha ya Kiswahili.

### 4.4.6 Nahau "Kenda Kombo" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Kwa kuangalia vijenzi vyake tunaona kuwa nahau hii imejengwa na maneno mawili ambayo ni neno "**kenda"** ambalo liko katika kategoria ya kitenzi lenye maana ya kutembea na neno "**kombo** " liko katika kategoria ya nomino ambalo ni jina la mtu kwa hivyo maana ya jumla ni **tendo la kutembea liliotendwa na mtu anayeitwa kombo**. Lakini maana yake kama inavyotumika katika Kiswahili kutokana na mtazamo wa nadharia ya maana kimatumizi na nadharia ya maana kimuktadha nadharia hii itakuwa na maana ya ***kukosea au kufanya jambo kinyume na inavyotakiwa***. Hapa panaonekana utata uliodhahiri baina ya maana ya kimuktadha na maana inayotokana na maneno yaliyojenga nahau wenyewe. Watu wanaotumia maana hizi hawatofahamiana na kwa kweli watakosa mawasiliano fanisi. Hivyo matumizi ya maneno yaliyoko katika kipengele cha nahau yanaleta utata kwa watu wasio weledi wa lugha kwani wao huelewa maana ile iliyoko wazi (yaani inayoonekana kupitia maumbo ya maneno).

### 4.4.7 Nahau "Andika Meza" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Maana ya nahau hii kama inavyotumika katika Kiswahili ni ***kuweka chakula juu ya meza***. Hata hivyo kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau hii maana yake itakuwa ni ***kutumia meza kama kifaa kinachotumika kwa kuandikia kama vile linavyotumika daftari au ubao wa kuandikia ndani ya daeasa.*** Hivyo basi matumizi ya nahau hii mbele ya mgeni wa lugha ya Kiswahili yanaweza kuleta ukakasi wa kimakusudio na kwa hivyo kushindikana kupatikana ujumbe uliokusudiwa. Hii ni kwa sababu mgeni wa lugha huielewa maana ya sentensi au aya kulingana na maneno yaliyoijenga aya au sentensi hiyo. Inawezekana ikawa hajui kabisa kama kuna maana iliyofichikana kwa baadhi ya maneno au vifungu vya maneno. Jambo hili linaweza kusababisha mawasiliano fanisi baina ya mwenyeji wa lugha na mgeni wa lugha asiyetambua maana za ndani za nahau.

### 4.4.8 Nahau "Kuchungulia Kaburi" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Mgeni wa lugha yoyote mara nyingi anapojifunza lugha hutaka kuelewa lugha hiyo ili aweze kupata urahisi wa kuwasiliana na wenyeji wa lugha. Kwa hatua za mwanzo ujifunzaji wake wa lugha huwa ni wa juu juu tu na sio kwa undani kabisa. Mara nyingi mjifunzaji lugha huzitizama maana kwa kuzingatia maana za maneno yaliyojenga maneno, tungo au sentensi husika. Kwa mtu kama huyu mfano wa nahau kama hii **"*kuchungulia kaburi*"** huijengea tafsiri kuwa ni ***kitendo cha kuangalia ndani ya shimo lililotayarishwa kwa ajili ya kuingizwa mwili wa mtu aliyefariki***. Lakini katika Kiswahili kwenye muktadha wa matumizi nahau hii ina maana ya

***kuumwa sana au kuwa mahtuti kutokana na maradhi au ajali***. Kwa hivyo yanapotumika maneno haya katika kipengele cha nahau mgeni wa lugha akawa anahusika nayo basi hawezi kujua mantiki iliyokusudiwa katika maneno hayo. Mgeni wa lugha hatoweza kuuelewa muktadha wa kifungu hiki cha maneno kwani yeye ana uwezo wa kutafsiri maneno kwa kuyaangalia kwenye maana zake za kawaida. Kwa mfano wenyeji wa lugha ya Kiswahili wanaposema Juma sasa yupo vizuri, lakini aliwahi ***kuchunguliwa kaburi,*** wao wenyewe wataaelewana, lakini mgeni wa lugha atapata shida katika kuelewa muktadha na kufahamu makusudio. Kwa muktadha huo mawasiliano fanisi hukosekana. Mtafiti ameongozwa na nadharia ya maana kimatumizi na maana kimuktadha katika kutoa maana ya nahau hapo juu. Maana imetolewa kutokana na muktadha wa kimazingira na kijamii. Katika muktadha wa kimazingira ya kinahau na uelewa wa utamaduni wa Kiswahili, ***kuchunguliwa kaburi*** maana yake ni ***kuumwa sana karibu na kifo***, kwa mtazamo wa kibinaadamu.

### 4.4.9 Nahau "Amevunja Ungo" Inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Maana ya nahau hii kama inavyotumika katika Kiswahili ni ***amepata ukubwa au utu uzima***. Ametokwa na damu ya hedhi kwa mara ya mwanzo katika maisha yake. Jambo hili linaashiria utayari wake wa kimaumbile. Anaingia kwenye utu uzima wa maisha ya kimwili. Hii ni maana yake kimatumizi. Ubainishaji wa maana kama huu unaendana kabisa na nadharia mbili zilizoteuliwa, Nadharia ya maana kimatumizi na ile inayoangalia maana kimuktadha. Lakini kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau maana yake ingekuwa ***ni kuharibu kifaa kinachotumika kupepetea nafaka.*** Muktadha wa maana yake kimatumizi si rahisi hata kidogo kueleweka na wageni wa

lugha. Hii ni kwa sababu mgeni wa lugha ingawa anaweza kuelewa taratibu za uzungumzaji wa lugha kwa kuitambua sarufi na kanuni za kuunda sentensi hawezi kuelewa maana ya ndani ya sentensi ila huelewa maana kwa kuangalia maumbo ya maneno yaliyounda sentensi hizo. Jambo hili kwa kweli husababisha kutokuwepo maelewano kati ya wenyeji lugha wanaofahamu utamaduni wa lugha yao na wageni wanaojifunza lugha wasiozitambua tamaduni za lugha hiyo.

### 4.4.10 Nahau "Ameacha njia" Inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

***La pili ni njia lenye maana ya sehemu inayotumika kupitia***. Maana ya nahau hii kama inavyotumika katika Kiswahili ni "***Amepotea" . Kama maana ya nahau hii ingeangaliwa kwa kutupia macho*** viambajengo vya nahau yenyewe tungeona kwamba maana ya nahau hii ni kutembea bila kufuata sehemu maalumu ya kupitia. Hivyo mjuzi wa lugha na mtambuzi wa nahau anapotumia maneno kama haya anasababisha kizingiti cha kimawasiliano baina yake na mgeni wa lugha, hiyo banakosekana mawasiliano fanisi. Mgeni anashindwa kufahamuni nini hasa alichokikusudia au anaweza kutoa mlisho nyuma kinyume kabisa na lengo la mazungumzo hayo. Nadharia iliyotumika hapa ni ile ya maana kimatumizi ambayo inaibainsha maana kama wanacvyoitumia waongeaji wenyewe na sio kama ilivyowasilishwa kutokana na vijenzi vya lugha.

### 4.4.11 Nahau "Aliniunga Mkono" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Kwa kuzingatia vijenzi vya nahau hii maana yake itakuwa ni kwamba kuna mtu

ambaye ***aliunganisha mkono wanguambao ulikuwa katika vipande tofauti.*** Lakini kimuktadha wa kijamii, kama inavyofafanuliwa na nadharia ya maana kimuktadha maana ya nahau hii itakuwa ni ***"alikubaliana na mimi kimtazamo au kimawazo katika hoja au jambo fulani"*** .Kwa maana hiyo mwenye kujifunza lugha (mgeni wa lugha ) anaposikia matumizi ya nahau katika mawasiliano anaweza kudhani kuwa yale maneno yaliyotumika hayana maana moja (yana maana zaidi ya moja ) kama yalivyo maneno "'kata, kaa,shuka," kitu ambacho sio sahihi ila tu maana iliyokusudiwa hapa ni ya kisanaa na haieleweki ila kwa wale wanaoijua luhga kiundani. Nadharia ya kimatumizi inasisitiza kwamba maana ya neno katika lugha ni matumizi yake. Hivyo haina haja ya kuuliza neno hili lina maana gani bali angalia vipi neno hilo linavyotumika. Kwa muktadha huu tunasema kwamba nadharia hii imetusaidia kueleza maana ya maneno ameniunga mkono katika muktadha wa kinahau na siyo kuuliza maana ya neno kuunga na neno mkono lina maana ipi? Tunachoweza kuuliza kifungu hiki cha maneno katika muktadha wa jamii ya Waswahili kinatumika vipi? Hili pia linaenda sambamba na nadharia ya maana kimuktadha inayoangalia maana katika muktadha wa kimazingira na kijamii.

### 4.4.12 Nahau "Ameanguka mtungi" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Tukiangalia mjengeko wa nahau hii tunakuta kwamba imejengwa na maneno mawili ambayo moja ni kitenzi "***ameanguka***"lenye maana ya ***kutoka katika sehemu ya juu kwenda chini kwa bahati mbaya*** na neno la pili ni nomino ***"mtungi"*** lenye maana ya ***chombo ambacho zamani kikitumiwa kuekewa maji ili yawe baridi kwa ajili ya kunywewa***. Kwa mjengeko huo maana ya nahau hii ilitarajiwa iwe ni ***kudondoka***

***kutoka juu ya chombo*** ambacho ***zamani kikitumika kuwekea maji yapate baridi.*** Lakini kwa kuangalia maana ya nahau kama inavyotumika katika Kiswahili kupitia nadhari ya maana kimatumizi na nadharia ya maana kimuktadha nahau hii maana yake ni "tendo la ***mwanamme kupoteza nguvu za kiume".*** Kwa maana hivyo kutokana na kuwa maana ya nahau kama inavyotumika katika Kiswahili ni hiyo ni dhahiri kuwa matumizi ya nahau katika mawasiliano yanaweza kuwamisha mawasiliani fanisi kwa mgeni wa lugha. Hii ni kwa sababu, mgeni wa lugha yeye hujifunza sarufi ya lugha tu na nahau hazitoi maana ya kisarufi bali maana zke huwa ni za kifasihi.

### 4.4.13 Nahau "Kutapikia sandani " inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Nahau hii maana yake katika Kiswahili ni ***kucheka tatizo aliojaliwa kuwa nalo mwaenzako na wewe bado uko hai***. Maana hii inaakisi kabisa nadharia teule zinazohimiza utoaji wa maana kimuktadha na kwa kuangalia maneno yaliyotumika kujenge umbo linalotolewa maana. Kama viambajengo vilivyotumika vingezingatiwa katika kutoa maana, kikundi hiki cha maneno kingefasiriwa Hili ni tendo la kutoa chakula ambacho tayari kilikuwa tumboni na kuchafua kitambaa kina chotumika kuvishiwa maiti. Kutokana maana hizi mbili kutokuwa na uhusiano hata mdogo tunaweza kusema kuwa pindi nahau hii ikitumia mbele ya mgeni wa lugha basi mgeni huuyu hatoambulia chochote katika mazungumzo hayo.

### 4.4.14 Nahau "Amaemlanda baba yake" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Nahau hii maana yake katika Kiswahili ni ***Kafanana na baba yake***. Lakini tukiangalia maana kwa kuzingatia maumbo ya maneno yaliyounda nahau hii maana yake ingekuwa ni ***kupita juu ya mwili wa baba yake .*** kwa hiyvo kutokana na kuwa nahau hutumia maana ya uficho ambayo kwa nahau hii ni ile ya mwanzo ambayo ni kufanana na baba yake basi matumizi ya nahau katika kuwasliana lazima yawe ni mawasliano kati ya mweledi wa luhga na mweledi wa lugha na sio kati ya mweledi na mgeni wa lugha kwani wageni wa lugha wanaweza kutofahamu kilichokusudiwa kwa sababu wao wanaelewa maana ya wazi na sio ile maana iliyojificha. Maana ya nahau zaidi inatafsiriwa kimatumizi jambo ambalo linaakisi nadharia teule ya maana kimatumizi.

### 4.4.15 Nahau " Ameukata" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Nahau hii imeundwa na neno moja ambalo liko katika kategoria ya kitenzi lenye maana ya ***kugawa katika sehamu ndogo ndogo kitu ambacho kilikuwa kizima.*** lakini kwa kuangali maana ya nahau hii kama inavyotumika katika Kiswahili ni" ***kufanikiwa kimaisha***" kwa hivyo kutokana na kuwa nahau hutoa maana ya uficho zinapotumiwa katika mawasiliano ni lazima mawasiliano hayo yawe kati ya mweledi wa lugha na mweledi wa lugha na sio mweledi na mgeni wa lugha wa kwani mgeni wa lughaanaweza kupata ukakasi juu ya ujumbe uliokusudiwa hii ni kwasababu wageni wa lugha hujifunza lugha kijuu juu tu na sio kiundani na nahau mara zote unaweza ukaiona ni ndogo na nyepesi kiumbo lakini ujumbe wake ni mkubwa na ni mzito. Kimuktadha na kimatumizi neno ameukata

lina maana ya kufanikiwa kimaisha na siyo kukigawa kitu katika vipande. Nadharia teule zimekuwa faafu katika kuakisi tafsiri ya neno ameukata kimuktadha

### 4.4.16 Nahau " Bao la Mkahawani"inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili

Maana ya nahau hii kama inavyotumika katika Kiswahili ni ***'Mwanamke Malaya***" (hachagui kila mtu ni wake ) Lakini tukiangalia maana ya nahau kwa kuangalia viambajengo vilivyounda nahau wenyewe bao la wageni ni '***sehamu inayotumika kukalia watu wakiwa katika mkahawa*** " kwa hivyo tukiangalia maana ya mwanzo tunaona kuwa endapo maneno haya yakizungumzwa mbele ya mgeni wa lugha hatoweza kuelewa mzungumzaji amekusudia nini hivyo hawezi kupata ujumbe kamili uliokusudiwa kwani yeye anaweza tu kufasiri ile maana ya pili ambayo ni maana ya wazi inayozingati maumbo ya maneno yaliyounda nahau hiyo. Nadharia ya maana kimatumizi imemsaidi mtafiti kukubaliana na maana ya nahau kama Waswahili wenyewe wanavyoitumia.

### 4.4.17 Nahau " Kata maini" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili

Kimatumizi katika lugha ya Kiswahili, nahau hii ina maana ya kupata maumivu makali na hisia mbaya katika moyo. Ufahamu wa maana hii unatofautiana sana na maana inayoweza kupatikana kwa kuzingatia viambajengo vya nahau yenyewe. Kwa mtazamo huu '***kata ini'*** maana yake ni ***"kukatakata na kukigawa sehemu ndogo ndogo kiungo cha kiumbe hai kinachoitwa ini".*** Wakati wa matumizi ya nahau hii panaweza pakatokea kutokuelewana baina ya wageni wa lugha ambao wanelewa

maana kutokana na vijenzi vilivyotumika na wenyeji wa lugha ambao wanaelewa maana ya nahau kimuktadha kama inavyoakisiwa na nadharia ya maana kimuktadha. Jambo hili bila shaka yoyote litakwamisha mawasiliano fanisi baina ya watumiaji wawili wa lugha. Mwenyeji wa lugha anayetambua utamaduni na muktadha wa kimatumizi na mgeni wa lugha anayejuwa maana za juu juu bila kuzingatia tamaduni za lugha na muktadha wa kimatumizi.

### 4.4.18 Nahau "Chomea utambi" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili

Kuchomea utambi kwa maana itokanayo na fasili ya maneno ni ***kuwasha moto na kuuchoma utambi kwa niaba ya mtu*** lakini katika muktadha wa kimatumizi kwenye lugha ya Kiswahili nahau hii inatumika kwa maana ya ***kumchongea mtu na kumsingizia jambo ambalo hanalo makusudi aingie hatiani na kuadhibiwa hasa na mkuu wa kazi.*** Mtazamo huu ndio ambao unakubaliana na nadharia ya maana kimatumizi na maana kimuktadha. Tofauti hizi za maana, hii iliyo katika ufahamu wa mgeni na ile iliyokusudiwa kiumuktadha, huweza kuwatenganisha wawili hawa wasiweze kuelewana kabisa. Mgeni huyu anaweza kuhisi kama kwamba anatengwa katika mazungumzo yale na kusudio la mazungumzo hayo ni kumsema kwa lugha asiyoielewa kwa makusudi ili yeye asielewe wanachozungumza. Dhana hiyo anayoweza kuijenga mgeni ni kinyume na ukweli wa mambo. Mazungumzo kama haya ni ya kawaida tu yasiyo unyanyapaa ndani yake ila tu ni kwa yule mjuzi wa lugha. Asiyejua lugha bila shaka hutatizika.

### 4.4.19 Nahau "Kaza buti" " inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha ya Kiswahili

Maana ya nahau hii katika Kiswahili ni ***kuongeza juhudi***. Hii ni maa ya kimuktadha na kimatumizi inayoendana na mtazamo wa nadharia zetu teule. Lakini maana ya nahau hii kwa ziangatia viambajengo vilivyounda nahau ni ***kufunga zaidi nyuzi za kiatu vya kuvika ambazo zilikuwa zimelegea***. Kwa hivyo maana hizi zinatofautiana, ila mwenye kujifunza lugha anaweza kudhani kwamba anatakiwa azidishe uimara wa kiatu chake kiepukane na kulegea ili kisije kikavuka hivyo, mawasiliano hapa yanatoa ujumbe ambao haukukusudiwa ila tu kwa sababu ya uwelewa finyu wa lugha mgeni wa lugha hatoweza kuzingatia maana ya ndani ya nahau. Kwa muktadha huu mawasiliano fanisi baina ya
mwenyeji na mgeni wa lugha.

### 4.4.20 Nahau "Ana Ndimi Mbili" Inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Kama inavyoeleweka ndimi ni neno linalowakilisha wingi wa neno ulimi (mchakato wa kifonolojia). Kwa muktadha huo nahau isemayo ***ana ndimi mbili"*** italeta maana ya kwamba ***anavyo viungo viwili vinavyoitwa ulimi.*** Iwapo maana ingetolewa kwa kuzingatia vijenzi vya ibara hii. Lakini hata hivyo nahau hii kwa kuzingatia maana yake kimuktadha kama inavyotumika katika Kiswahili maana inayokusudiwa ni ***mtu asiekuwa na msimamo katika mazungumzo yaani mwenye kugeuka geuka juu ya kauli zake.*** kwa hivyo maneno haya yanapotumika mbele ya mgeni wa lugha anaweza kuelewa kuwa kuna kiumbe fulani kina viungo viwili vya ulimi jambo

ambalo ni kinyume kabisa na makusudio ya msemaji. Hapo sasa mawasiliano fanisi, baina ya mweledi wa lugha ya Kiswahili na mgeni wa lugha lazima yakosekane.

### 4.4.21 Nahau "Kujipalia Makaa" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Nahau hii katika Kiswahili inatumika kwa maana ya ***kujitia matatizoni,*** ila tukiangalia maana yake kwa kuzingatia viambajengo vilivyoiunda nahau wenyewe ingekuwa na maana ya ***kupaa vipande vya kuni vilivyowashwa moto kwa ajili yake, au kujisogezea makaa ya moto kwa ajili ya kujiunguza*** Matumizi ya nahau kama hiii katika mazingira ya watu wasiolewa lugha kunaweza kufanya kutokuwepo mawasiliano fanisi baina ya wenye lugha na wageni wa lugha. Wageni wa lugha wanaweza kushindwa kuelewa kile kinachoongelewa na hivyo hupelekea kutenda tendo kinyume na ilivyotarajiwa kutokana na kutafsiriwa kusiko kwa usahihi. ***Kujipalia makaa*** kwa wenyeji wa lugha kuna maana ya ***kujiingiza ndani ya matatizo***, ilhali jambo hilo lina maana ya kujisogezea moto na kujiunguza kwa wale wanaotafsiri kwa kutumia vijenzi vya maneno (wageni wa lugha). Maana ya nahau hii kimatumizi na kimuktadha inaweza kukubalika kwa kuzingatia nadharia zetu teule. Nadharia ya maana kimatumizi kwa upande mmoja na nadharia ya maana kimuktadha kwa upande wa pili.

### 4.4.22 Nahau "Kupigwa fyagio la chuma" inavyoweza Kukwamisha Mawasiliano kwa Mgeni wa Lugha

Kimuktadha na katika matumizi kwenye lugha ya Kiswahili, maana ya nahau *"**Kupigwa fyagio la chuma**"* ni ***kufukuzwa kazi***. Maana hii imekuja kimatumizi na

kimuktadha na siyo kwa kuangalia maana za maneno yaliyojenga nahau wenyewe. Ucambuzi huu unaakisi moja kwa moja nadharia zetu teule. Hata hivyo maana ya nahau hii hii kwa kuzingatia viambajengo vilivyoijenga ni ***kutumia kifaa kinachotumika kwa kufyagilia ambacho kimetengenezwa kwa chuma kama kifaa cha kupigia kama vile itumikavyo bakora au silaha nyengine.*** Hali halisi inaonesha kwamba, mgeni wa lugha akisikia nahau hii ikitumika basi yeye anachoelewa ni ile maana ya vijenzi vya nahau, jambo ambalo halitompa mawasiliano fanisi na hatoelewa kabisa makusudio ya nahau wenyewe. Maana ya kimafumbo mgeni wa lugha kwake itakuwa ngumu na ngeni. Kwa sababu hiyo mawasiliano fanisi kati yake na mweledi wa lugha na mtambuzi wa matumizi ya nahau hayatokuwepo.

## 4.5 Hitimisho la Sura

Sura hii imewsilisha na kuchambua data zilizokusanywa kupitia mbinu dodoso, mahojiano na usomji makini .Uchambuzi wa data hizo umezingatia malengo mahsusi ya mada husika. Ambapo kutokana na majibu ya watafitiwa matafiti ameweza kubainisha nahau mbali mbali ambazo aliweza kuzigawa katika makundi tofauti makundi hayo ni kama vile nahau zinazohusiana na mila na desturi za jamii, Nahau zinazohusu subra na uvumilivu, Nahau zinazohusu dini na imani, nahau zinazohusu maswala ya kielimu, Nahau zinazohusu manbo ya maadili, Nahau zinazohusu juhudi katika kazi, Nahau zinazohusu choyo na usaliti na nahau zinazohusu ushirikiano. Pia sura imeonesha uchambuzi wa maana za nahau kipragmatiki na maana za nahau kwa kuzingatia viambajeno vilivyounda nahau. Vile vile utafiti huu kupitia sura hii umeweza kubainisha jinsi nahau zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha ya Kiswahili . Sura inayofuata itatoa majumuisho ya kazi nzima kwa kuanza

kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho, mchango wa utafiti huu, mapendekezo ya maeneo yanayohitaji kufanyia utafiti.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHUTASARI HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha majumuisho ya jumla ya tatizo la utafiti huu unaohusu nahau za Kiswahili jinsi zinavyokwamisha Mawasiliano fanisi kwa Wageni wa lugha ya Kiswahili, vipengele vilivyohusiswa na sehemu hii ni muhutasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo ya maeneo yanayohitaji kuyafanyia utafiti na hitimishola sura nzima.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi nahau za Kiswahili jinsi zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha .Utafiti huu ulifanyika uwandani na Maktabani. utafiti ulikuwa na jumla ya sura tano. Katika sura ya kwanza kulikuwa na utanguliziwa jumla wa utafiti. Utangulizi huu umebainisha usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti. Ambapo sura ya pili imeonesha kazi tangulizi ambazo mtafiti amezipitia zinazoshabihiana mada ya utafiti huu kitu amabacho kilimwezesha mtafiti kugundua mwanya ambao ndio uliosababisha ufanyikaji wa utafiti huu kutokana na kuwa mada husika haijafanyiwa uchunguzi wa kina.

Pia katika sura hii zimefafanuliwa nadharia za maana katika matumizi na nadhara za maana katika muktadha ambazo ndizo zilizomuongoza mtafiti wa utafiti huu, pamoja pengo la utfiti. Sura iliyofuata ambayo ni sura ya tatu imekusanya vipengele kama vile muundo wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, data na aina zake,

njia zilizotumika kukusanya na kuchambua data pamoja na maadili ya utafiti. Sura ya nne iliwasilisha na kuchambua data zilizokusanywa toka uwandani na maktabani ambazo zilijibu maswali ya utafiti kwa ajili ya kufikia malengo ya utafiti. Sura ya tano ndiyo sura ya mwisho kwa utafiti huu ambayo inatoa hitimisho la utafiti mzima pamoja na  mchango wa utafiti. Pia sura inatoa maoni na mapendekezo kuhusu tafiti zinazoweza kufanywa ili kuendeleza utafiti huu.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti kwa Kila  Lengo

### 5.3.1 Lengo la Kwanza

Lengo hili liliongozwa na swali lisemalo ni zipi nahau za Kiswahili? Swali hili lilijibika kwa kuorodhesha nahau za lugha ya Kiswahili kama zilivyooneshwa katika UK 29-32 Mtafiti amegundua kuwa katika kiswahili kuna kipengele cha nahau ambapo kuna nahau zinazowakilishwa kwa neno moja tu na pia nahau zinazowakilishwa kwa vikundi vya maneno (virai). Pia nahau hizo zimegawika katika makundi tofauti ambayo ni kama naahau zinazohusu mila na dasturi za jamii, nahau zinazohusu mambo ya dini na imani,nahau zinazohusu ushirikiano, nahau zinazohusu juhudi katika kazi, nahau zinazohusu choyo na usaliti,nahau zinazohusu mambo ya maadili, nahau zinazohusu masuala ya kielimu.

### 5.3.2 Lengo la Pili

Lengo  hili liliongozwa na na swali lisemalo  ni maana zipi za nahau ni za kipragmatiki na maana zipi za nahau ni zenye kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau hizo. Katika  kujibu swali hili mtafiti aligundua nahau za Kiswahili kuwa hutoa maana iliyofichika na  na maana ya wazi. Mfano

#### 5.3.2.1 Maana Iliyojificha

**N:** Amevunja ungo

**M:** Amepata ukubwa

**N:** Kaza buti

**M:** Ongeza juhudi

#### 5.3.2.2 Maana Iliyo Wazi

**N :** Amepata jiko

**M:** Amemiliki sehemu au kifaa cha kupikia

**N:** Bao la mkahawani

**M:** Kifaa kinachotumika kukalia watu wakiwa mkahawani.

### 5.3.3 Lengo la Tatu

Lengo la tatu liliongozwa na swali lisemalo ni jinsi gani nahau za Kiswahili zinakwamisha mawasliliano kwa wageni wa lugha?. Swali hili lilijibika kwa mtafiti kunukuu baadhi ya nahau na mbazo alizitolea ufafanuzi wa maana kama zinavyotumika katika Kiswahili na maana kwa kuzingatia vijenzi vya nahau yeyewe na kuonyesha jinsi ambayo mgeni wa lugha anavyoweza kukwama kimawasiliano kutokana na sababu zifuatazo:-

- Nahau zinatoa maana za uficho
- Nahau maana zake haziko wazi
- Nahau hazitoi maana kisarufi
- Wageni wa lugha wanafahamu maana ya msingi tu
- Wageni wa lugha hawana ufasaha wa kutosha wa lugha

- Maumbo ya nahau ni tofauti na maana yenyewe (maana za nahau haizingazatii maumbo ya maneno).

### 5.4 Matokeo ya Jumla

Kwa ujmla mtafiti wa utafiti huu amegundua kuwa lugha Kiswahili ni pana katika matumizi yake kwani kuna baadhi ya vipengele vya lugha viko katika utamaduni zaidi wa lugha kwa sababu inaonyesha wanaojifunza lugha mbali na jitihada zao za kutaka kuielewa lugha hii inafikia wakati kuna mambo hawawezi kuyaelewa kwa kujifunza kwao lugha kijuu juu ila wanalazimika wasome lugha kiundani katika vipengele vyote vya isimu na fasihi na sio washughulikie upande mmoja tu jambo ambalo litapelekea kushindwa kuielewa lugha hiyo. Pia utafiti umegundua kuwa kuna mambo ambayo yanapelekea matumizi ya nahau yasababishe kukwama kwa mawasiliano kwa wageni wa lugha ambayo ni kama yafuatayo:- Kwanza Wageni wa lugha hujifunza zaidi sarufi ya lugha , vile vile wageni wa lugha hawana ufasaha wa kutosha wa luhga, Pia kwa vile lugha inakuwa inahusu utamaduni fulani hivyo wageni wa lugha hushindwa kuyaelewa baadhi ya mambo yanayohusu utamaduni, hata hivyo nahau hazitoi maana kisarufi. Pia pamoja na kuwa utafiti ulikuwa na lengo la kuchunguza jinsi nahau za Kiswahili zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha hiyo ila matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa nahau hazikwamishi mawasiliano kwa wageni wa lugha tu bali pia na wazawa wa lugha hukabiliwa na tatizo hili. Hii ni kwa sababu nahau hazitumiki mara kwa mara katika mazungumzo ya kila siku.

## 5.5 Mchango wa Utafiti

Kutokana na matokeo ya uchunguzi uliofanywa maoni yafuatayo yanapendekezwa:-
Wanajamii watumie kwa kiasi kikubwa nahau katika mawasiliano ili wageni nao waweze kuzielewa na wasione tabu kukaa na kuzungumza na wageni ili wafahamu mengi zaidi. Vile vile katika taasisi za ukuzaji lugha kwa mfano TAKILUKI, TATAKI na nyenginezo kuwekwe mikakati maalumu kuhusu ufundishaji wa nahau kwa wageni badala ya kuwafundisha kiswahili cha kawaida tu.Taasisi hizo pia ziandae majarida, vitabu na makamusi mbali mbali yenye nahau na maana zake. Pia katika mashule nahau zisomeshwe kwa kiwango kikubwa pamoja na umuhimu wa matumizi yake. Vile vile wageni wafahamishwe kwamba katika Kiswahili kuna matumizi ya maneno kulingana na makundi na muktadha pia .Hata hivyo watunzi wa vitabu nao washajiishwe kutumia nahau kwa wingi katika kazi zao. Na mwisho weledi wa lugha wanapotumia nahau katika mawasiliano kisha wazifafanue kulingana na wahusika wanaosikiliza ujumbe.

## 5.6 Mapendekezo kwa Tafiti Fuatishi

Matokeo ya utafiti huu yameweza kutoa mwanga unaoonesha iko haja ya kufaywa zaidi tafiti mbali mbali kama ifuatavyo:-

Watafiti wanayo nafasi ya kuchunguza nahau ili kubainisha maana na umuhimu wake katika matumizi ya watumiaji wazawa na wageni. Pia tafiti zifanywe kuchunguza njia gani zitumike zitakazoepusha kukwama kwa mawasiliano kutokana na matumizi ya nahau. Vile vile utafiti ufanyike kuchunguza ubora na udhaifu wa matumizi ya nahau katika mawasiliano.

## 5.7 Hitimisho

Sura hii inahusu ukamilishaji wa utafi mzima. Ambapo sura imeanza kwa kutoa muhutasari wa utafiti, ukifuatiwa na matokeo ya utafiti, pia sura imeonesha mchango wa utafiti, baadae yametolewa mapendekezo ya maeneo yanayotakiwa kufanyiwa utafiti na mwisho hitimisho la sura nzima .

**MAREJELEO**

Adam, J. & Kamuzora, F. (2008). Research Methods for Buisness and social studies. Mzumbe Book Project, Morogoro, Tanzania.

Alhabib, E. (2012). *Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Taarab*. Tasnifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

BAKIZA, (2008). *Utamaduni wa Mzanzibari*, Zanzibar.

Besti, J. W. & Kahn, J. V. (1993). *Research in Education*. United State of *America*. Allyn and Bacon.

Cozby, P. C & Bates, S. C. (2012). *Method in Behavioral Science Research.* (11th Ed). New Youk: Mc Graw - Hill.

Chum, H. (1982). *Desturi na Mila Zetu*. Arusha: East Africa Publication Limited.

Enon, J.C(1998). *Educational Research*; *Statistics and Measurement.* Kampala: Makerere University Press.

Hassan, A.U .(2013). *Dhima ya Methali katika Jamii ya Wapemba*. Chuo Kikuu cha UDOM.

Kiiza, J. P. (2004). Semi Fani ya Fasihi Simulizi, *Mulika* N. 12. Dar es Salaam: TUKI.

Kitiso, J. (1988). *Muundo wa Lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.

Kombo, D. K & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and thesis Writing*. *An Introduction.* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2008). *ResearchMethodology; Methods and Techniques*. New Delhi: New Age. International Publishing Limited.

Mahenge, P. (2009). Semi zitumikazo kwenye tiketi za daladala, *Mulika* Na 29 na 30. TATAKI.

Massamba, M. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mauya, M. (2006). Maandishi katika Vazi la Kanga wanazovaa Wanawake. Tasnifu ya M.A Kiswahili .Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Mulokozi, M. M. (1989). Tanzu za Fasihi simulizi. *Mulika* 21:1-24, Dar es Salaam: TUKI.

Mwansoko, H. (1991). *Mtindo wa Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam Press.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia kwa Sekondari vyuo vy kati na vyuo Vikuu.* Dar es Salaam: Educational Publishers (T) Ltd.

Mauya B, A. (2006). *Semi maana na matumizi* Chuo Kikuu cha Dar es Salam

Mohamed, H. A. (2016) *Maana za Majina ya Watu wa Pemba katika Lugha ya Kiswahili*. Tasnifu ya M.A Kiswahili .Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. ( 1996). *Fasihi ya Kiswahili* Chuo Kikuu Huria Cha Dar –es-Salamu.

Mnata. R. (2014). Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili. Dodoma, Tanzania.

Nassor, H. J. (2016). *Semi zilizoandikwa kwenye vyombo vya safari vyaa Baharini Kisiwani Pemba*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ndungo, C. M. & Waful, R. M. (1993). Tanzu za Fasihi Simulizi. University of Nairobi.

Nunuu, A.M (2013) *Mtazamo wa Wanafunzi na Walimu kuhusu Matumizi ya LUGHA Tandawazi katika Kiswahili*.Tasnifu ya M.A Kiswahili .Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Omari, C. K & Mvungi, M (1981). *Urithi wa Utamaduni wetu*. Dar es salaam, Tanzania Publishing House. .

Kaduguda, R., Kiango, J & Ipara, T. (2015). *Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha kwanza.*

Sengo T.S.Y.M (2009) *Sengo na fasihi za kinchi* Dar es salaam. AERA Kiswahiki Research Products

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988). *Kiswahili Sekondari*. Dar es Salaam: TUMI.

TAKILUKI, (1981) *Misingi ya Nadharia ya Kiswahili*. Stockholm: Arlovs.

TAKILUKI, (1981) *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Stockholm: Arlovs.

TUKI, (2010) *English-Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Walliman, N. (2011). *Research Methods:* London: Routledge.

Mulokozi, M. M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi, *Mulika* 21,1-24. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Uledi, F. M. (2012). *Muundo wa Lugha katika Methali na Vitendawili kwa jamii ya Wamakunduchi.* Wilaya ya Kusini Unguja. Chuo Kikuu Cha UDOM.

Wamitila, K. W. (2013). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wanjala.F.Simiyu (2013) *Kitivo cha Fasihi Simulizi kwa Shule na Vyuo na Ndaki.* Chuo Kikuu cha Kenya Nairobi.

Waziri, J. B. (2005). *Tofauti za kimsamiati kati ya Kipemba na Kikojani katika Mawasiliano ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba*.Tasnifu ya M.A Kiswahili .Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO Na: 1

**Uchambuzi wa maana za Nahau kama zinavyotumika katika Kiswahili (Kipragmatiki)**

| s/na | **Nahau** | **Maana ya Nahau Kipragmatiki** |
|---|---|---|
| 1 | Ana ndimi mbili | Hana msimamo (mnafiki) |
| 2 | Joka la mdimu | Mtu asiye na haja na kitu lakini anawazuia wenzake wasifaidike na kitu hicho |
| 3 | Amemlanda babae | Kafanana na baba yake |
| 4 | Kutapikia sanadani | Kumcheka mwenzako aliyefikwa na tataizo wakati na wewe uko hai |
| 5 | Kuanguka mtungi | Hali ya mwanamme kukosa nguvu za kiume |
| 6 | Mkono mfupi | Mbakhili |
| 7 | Kuchimba dawa | Kujisaidia haja ndogo au kubwa hasa katika mazingira ya vichakani au maporini. |
| 8 | Ana miguu mirefu | Mtu mwenye uwezo wa kutembea na kufika anapotaka bila ya matatizo |
| 9 | Ameukata | Amefanikiwa kimaisha |
| 10 | Amekula miguu ya kuku | Mtu anaetembea sana |
| 11 | Jamvi la wageni | Yupo kwa ajili ya wageni |
| 12 | Bao la mkahawani | Kila mtu ni wake hachagui (mwanamke au mwanamme Malaya) |
| 13 | Mkono wazi | Mkarimu |
| 14 | Amekula kichwa cha samaki | Mtu mwenye uzito wa kufahamu |
| 15 | Amepata ua | Amepata mwanamke mzuri |
| 16 | Amepiga ndoo teke | Amekufa |
| 17 | Kukanyaga nyaya | Kupata ukimwi |
| 18 | Amepiga mbizi | Amefanikiwa kimaisha |
| 19 | Kushika kitabu | Kusoma (kuwa mwanafunzi) |
| 20 | Kupaka mafuta kwa nyuma ya chupa | Kudanganya (kukejeli) |
| 21 | Kuzunguka mbuyu | Kutoa rushwa |
| 22 | Ana mkono mrefu | Mtu mwenye uwezo wa kupata kitu popote hata kama kiko mbali |
| 23 | Kaza buti | Ongeza juhudi |
| 24 | Mja mzito | Mwanamke mwenye mimba |
| 25 | Ana kichwa kikubwa | Ana akili nyingi |
| 26 | Amejifungua | Amezaa |
| 27 | Ana jicho la nje | Muhuni anaependa mwanamke huyu na yule |
| 28 | Amekuwa popo | Hana msimamo |
| 29 | Kachonga mwiko | Ameoa |

| | | |
|---|---|---|
| 30 | Kupiga moyo konde | Kijitolea muhanga (kuvumilia) |
| 31 | Anapiga domo | Anazungumza sana |
| 32 | Ana mkia wa mbuzi | Ana kitu ambacho hakimtoshi yeye wala hakiwafai wenzake |
| 33 | Kata maini | Umia moyoni |
| 34 | Ameasi ukapera | Ameoa |
| 35 | Amevuta kamba | Amefariki |
| 36 | Ana mkono wa buli | Mtu aliyekuwa chake hakipatikani (mbakhili) |
| 37 | Amekula chumvi nyingi | Ameishi miaka mingi |
| 38 | Amemwaga unga | Amepoteza ajira (Amefukuzwa kazi ) |
| 39 | Kupigwa kipapai | Kufanyiwa ushirikina (kulogwa ) |
| 40 | Kachanganya mawazo | Hakufahamu |
| 41 | Kupigwa fyagio la chuma | Kufukuzwa kazi |
| 42 | Kula mlugura | Kula rushwa |
| 43 | Ana mkono mkono | Mwizi |
| 44 | Kaza kamba | Ongeza bidii |
| 45 | Piga vijembe | Sema kwa lugha ya mafumbo |
| 46 | Amelala chali | Amefariki dunia |
| 47 | Kakunja uso | Amekasirika |
| 48 | Kumbatia rufani | Kujitia matatizoni |
| 49 | Kenda kombo | Kenda kinyume/kakosea |
| 50 | Kuchungulia kaburi | Kuumwa sana (mahtati) |
| 51 | Ana mguu mzito | Ana tende |
| 52 | Kuchomea utambi | Kujenga ushawishi kwa ajili ya kumfitinisha mtu |
| 53 | Kujikaza kisabuni | Kufanya jambo huku ukiwa unaumia |
| 54 | Amevunja chupa | Mjamzito aliyeonyesha dalili zakuwa si muda mrefu atajifungua ( kutokwa na maji ya uzazi ) |
| 55 | Ameaga dunia | amefariki |
| 56 | Piga maji | Kulewa |
| 57 | Kushika usukani | Kuongoza hasa katika mashindano |
| 58 | Mezea mate | Kutamani |
| 59 | Yuko msalani | Yuko chooni |
| 60 | Andika meza | Weka chakula katika meza |
| 61 | Kujipalia makaa | Kujitia matatizoni |
| 62 | Pita njia za panya | Fanya jambo bila kufuata taratibu za kisheria |
| 63 | Ona cha mtema kuni | Pata adhabu kali (usumbufu) |
| 64 | Lisha nyama ya ulimi | Tumia lugha tamu katika kushawishi jambo |
| 65 | Kufa na tai shingoni | Kukwepa aibu |
| 66 | Kufa moyo | Kukata tamaa |
| 67 | Kunja virago | Hama |
| 68 | Kata maini | Umiza sana |
| 69 | Amefurutu ada | Amezidisha kima cha malipo au amefanya jambo kuzidi kiwango kilichotarajiwa |
| 70 | Chapua mguu | Zidisha mwendo |
| 71 | Amewacha njia | Amepotea |
| 72 | Mama huruma | Mwanamke kahaba /Malaya |

| | | |
|---|---|---|
| 73 | Kupigwa kibuti | Kukataliwa na mpenzi wako |
| 74 | Amekufa kikondoo | Amekufa kishujaa |
| 75 | Kunawa mikono | Kujitoa kwa hiari katika jambo |
| 76 | Kumkalia mtu kitako | Kumsema /kumsengenya mtu |
| 77 | Ana roho ya korosho | Ana roho mbaya /mkorofi |
| 78 | Kukata shingo | kutokubali jambo |
| 79 | Aliniunga mkono | Alikubaliana na mimi |
| 80 | Ana kijicho | Mtu mbaya |
| 81 | Amekula debe | Amepata hasara |
| 82 | Kutia fora | Kufanya jambo kupita kiasi |
| 83 | Kata shauri | Toa uamuzi |
| 84 | Amevunja ungo | Kitendo cha kutoka damu ya hedhi kwa mara ya kwanza na kwa hivyo kubadilika kutoka hatua ya utoto na kuingia utu uzima |
| 85 | Amepata jiko | Ameoa |

## KIAMBATANISHO Na:2

***Uchambuzi wa maana za Nahau kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda Nahau***

| s/n | Nahau | Maana ya nahau kwa kuzingatia viambajengo vilivyounda nahau |
|---|---|---|
| 1 | Ana ndimi mbili | Ana viungo viwili vinavyoitwa ulimi |
| 2 | Joka la mdimu | Nyoka mkubwa anayekaa chini ya mdimu |
| 3 | Amemlanda baba yake | Kapita juu ya mwili wa baba yake |
| 4 | Kuanguka mtungi | Kudondoka kitoka juu kwa chombo ambacho zamani kikitumika kuhifadhia maji ili yawe baridi |
| 5 | Kutapikia sandani | Kuchafua nguo inachotumika kuvishia mtu maiti wakati wa kumuandaa kwa ajili ya mazishi |
| 6 | Mkono mfupi | Kiungo cha mwili kinachotumika kushikia na kufanyia kazi chenye ufupi usio wa kawaida |
| 7 | Kuhcimba dawa | Kufukua ardhi ili kupata mzizi wa mti ambao unatumika kwa ajili ya matibabu |
| 8 | Mkono wazi | Kiungo cha mwili kinachotumika kufanyia kazi ambacho kimekunjuliwa |
| 9 | Ameukata | Amegawa sehemu ndogo ndogo kitu ambacho kilikuwa kizima |
| 10 | Amekula miguu ya kuku | Amekula viungo vya ndege anaefugwa majumbani vinavyotumika kwa kutembelea |
| 11 | Amekula kichwa cha samaki | Amekula kichwa cha kiumbe wa baharini anaetumika kwa kitoweo |
| 12 | Ana miguu mirefu | Mtu mwenye miguu iliyorefuka kuliko kawaida ya watu wengine |
| 13 | Jamvi la wageni | Kifaa kinachotandikiwa wageni ili wakalie |
| 14 | Bao la mkahawani | Sehemu inayotumika kukalia watu wakiwa katika mkahawa |
| 15 | Amepata ua | Amemiliki kiungo cha uzazi cha mti kinachoonesha dalili ya kuzaa kwa matunda au ukomavu wa mti |
| 16 | Amepiga ndoo teke | Amepindua chombo kinachotumika kutekea au kuwekea maji |
| 17 | Kukanyaga nyaya | Kakanyaga vifaa vinavyotumika kusafirishia umeme kutoka kiungo kimoja hadi kingine |
| 18 | Kupiga mbizi | Kuzamia katika maji |
| 19 | Kushika kitabu | Kukamata kitabu |
| 20 | Kupaka mafuta kwa nyuma ya chupa | Kitendo cha kueneza mafuta kwa kutumia sehemu ya nje ya chupa |
| 21 | Kuzunguka mbuyu | Kitendo cha kuzunguka mti mkubwa mnene unaoitwa mbuyu |
| 22 | Ana kicwa kikubwa | Umbo la kichwa chake ni kubwa kuliko kawaida |
| 23 | Ana jicho la nje | Kiungo chake cha mwili kinachotumika kwa kuonea kimetoka nje |
| 24 | Kaza buti | Funga nyuzi za viatu vya kuvika ambavyo vimelegea |
| 25 | Mja mzito | Mtu mwenye uzito usio wa kawaida |

| | | |
|---|---|---|
| 26 | Amejifungua | Ameepukana na kizuizi fulani |
| 27 | Amekuwa popo | Amekuwa na umbo la ndege anaening'inia katika mti wakati akilala usingingizi |
| 28 | Ana mkia wa mbuzi | Ana kiungo cha mnyama anaeitwa mbuzi ambacho kinatumika kujipungia wadudu wasimkere |
| 29 | Kachonga mwiko | Katengeneza kifaa cha mbao ambacho kinatumika kukorogea chakula wakati wa kupika |
| 30 | kupiga moyo konde | kutumia kiungo cha mkono |
| 31 | Anapiga domo | Kitendo cha kugonga kiungo cha kiumbe kinachoyumika kuzungumzia lugha |
| 32 | Kata maini | Tenganisha kiungo cha kiumbe kinachoitwa ini kutoka mwilini |
| 33 | Kufa moyo | Kitendo cha kupoteza hisia katika moyo |
| 34 | Kunja vilago | Kusanya nguo kuu kuu |
| 35 | Ameacha njia | Kutembea bila ya kufuata sehemu maalumu ya kupita |
| 36 | Kupigwa kibuti | Kitendo cha kupigwa kwa kutumia kiatu kidogo cha kuvika |
| 37 | Amekufa kikondoo | Amekufa kama anavyokufa mnyama anaeitwa kondoo |
| 38 | Kunawa mikono | Kusafisha mikono kwa kutumia maji |
| 39 | Kumkalia mtu kitako | Kuweka makalio juu  ya kiwili wili cha mtu |
| 40 | Ana roho ya korosho | Ana roho uenye umbo la tunda linaloitwa korosho |
| 41 | Kukata shingo | Kutenganisha kichwa na kiwili wili |
| 42 | Amefurutu ada | Amezidisha kima cha malipo |
| 43 | Mama huruma | Mzazi wa kike mwenye huruma |
| 44 | Aliniunga mkono | Aliuunga mkono uliokuwa umevunjika |
| 45 | Ana kijicho | Ana kiungo cha mwili ambacho kinatumika kwa kuonea ambacho ni kidogo kuliko kawaida |
| 46 | Amekula debe | Ameingiza mkebe tumboni kama anavyoingiza chakula |
| 47 | Kutia fora | Kuzidisha |
| 48 | Kata shauri | Kupinga mawazo yaliyotolewa na wengine |
| 49 | Ameasi ukapera | Kwena kinyume na taratibu za kijane |
| 50 | Amevuta kamba | Amefanya kitendo cha cha kuvuta kifaa kinachotumika kwa kufungia kitu |
| 51 | Amevunja ungo | Ameharibu kifaa kinachotumika kupepetea nafaka |
| 52 | Amepata jiko | Amemiliki kifaa au sehemu ya kupikia |
| 53 | Amekula chumvi nyingi | Amekula kitu kinachotengenezwa kwa maji ya bahari kinachotumika kuchapuzia chakula |
| 54 | Amemwaga unga | Amedndosha kitu kilicho katika hali ya chembe chembe ngo sana mfano wa vumbi |
| 55 | Kupigwa kipapai | Kutumwa tunda linaloitwa ppai kama kifaa cha kupigia (bakora) |
| 56 | Kachanganya mawazo | Kukusanya fikra za watu tofauti |
| 57 | Kupigwa fyagio la chuma | Kupigwa kwa kutumia kifaa cha kufyagilia kilichotengenezwa kwa chuma |
| 58 | Kula mlungura | Kula kitu kilichotengenezwa kwa mbao kilicho mfano wa ngoma |
| 59 | Kaza kamba | Kitendo cha kuzidisha kamba iwe imara katika |

| | | |
|---|---|---|
| | | sehemu ilipofungwa |
| 60 | Piga vijembe | Kitendo cha kugonga gona vijembe |
| 61 | Amelala chali | Amelala hali ya kuelekeza tumbo juu |
| 62 | Kakunja uso | Amefinya sehemu ya mbele ya kichwa |
| 63 | Kumbatia rufani | Kushikilia kitu kinachoitwa rufani kwa kutumia mikono pamoja na sehemu yote ya mbele ya mwili |
| 64 | Kenda kombo | Katembea mtu anayeitwa kombo |
| 66 | Kuchungulia kaburi | Kitendo cha kuangalia shimo linalo tarajiwa kuingizwa mwili wa kiumbe aliyefariki |
| 67 | Ana mguu mzito | Ana mguu wenye uzito usio wa kawaida |
| 68 | Kuchomea utambi | Kuwasha moto utambi kwa niaba ya mtu |
| 69 | Kujikaza kisabuni | Kustahamili bila uwezo mfano wa sabuni |
| 70 | Amevunja chupa | Amebomoa kifaa kinachotunika kuwekea vitu vyenye hali ya kimiminika |
| 71 | Ameaga dunia | Kitondo cha kutolea dunia mkono wa mwisho |
| 72 | Piga maji | Kitendo cha kuyagonga maji ama kwa mkono aua kwa kutumia kitu kchochote |
| 73 | Kushika usukani | Kukamata kifaa cha chombo cha usafiri kitachotumika kuelekezea chombo kiende upande fulani |
| 74 | Mezea mate | Kusukuma mate yaende tumboni kwa niba ya mtu au mbele ya mtu |
| 75 | Yuko msalani | Yuko katika kifaa kinachotumika kwa kuswalia |
| 76 | Andika meza | Tumia meza kama kifaa cha kuandikia kwa mfano buku au ubao |
| 77 | Kujipalia makaa | Kutoa vipande vya kuni vilivyochomwa moto kwa ajili yako au ukaviweka karibu yako |
| 78 | Pita njia za panya | Kitendo cha kupita katika sehemu wanazotumia kupita panya |
| 79 | Ona cha mtema kuni | Angalia kitu cha mtu mwenye kazi ya kukata miti kwa ajili ya kupikia |
| 80 | Lisha nyama ya ulimi | Mtilie mtu mdomoni kipande cha ulimi wa mnyama au binaadamu |

# KIAMBATIHO  Na 3

## DODOSO KWA WANAFUNZI

**Maelezo kuhusu mtafiti**

Mimi ni mwanafunzi halali wa chuo kikuu huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya "Nahau za Kiswahili sanifu jinsi zinavyokwamisha Mawasiliano fanisi kwa Wageni wa Lugha." Hivyo naomba ushirikiano mwema kotoka kwako.

**SEHEMU A : Maaelezo binafsi ya mtafitiwa**

Weka alama ya vyema [√ ] katika sehemu inayostahiki na toa maelezo katika sehemu inayohitaji maelezo

1Umri ____________________________________________

2) Mume [ ] Mke [ ]

3) Kiwango cha elimu

sekondari [ ] Chuo [ ]

4) Dhamana

Mwalimu [ ] Mwanafunzi [ ]

**SEHEMU B: Maswali**

1a) Jee! Umewahi kusikia kwamba kuna nahau katika kiswahili ?

Ndio [ ] Hapana [ ]

b) Kama jawabu ndio taja nahau za Kiswahili angalau tano

i)________________________________________________

ii) ________________________________________________

iii) ___________________________________________________________

iv) ___________________________________________________________

v) ____________________________________________________________

2) Eleza maana ya Nahau ulizozitaja hapo juu kama zinavyotumiwa katika Kiswahili

| | Nahau | Maana |
|---|---|---|
| i | | |
| ii | | |
| iii | | |
| iv | | |
| v | | |

3)Eleza maana ya nahau ulizozitaja katika na.1b kwa kuzingatia maumbo ya maneno yaliyotumika kuunda nahau hizo.

| | Nahau | Maana |
|---|---|---|
| i | | |
| ii | | |
| iii | | |
| iv | | |
| v | | |

4a)Katika hali ya kawaida inaonekana Nahau zinatumia lugha ya uficho. Je! Unafikiri

matumizi ya Nahau yanaweza kupelekea ugumu wa mawasiliano kwa wageni wa lugha ya Kiswahili?

Ndio [ ] Hapana [ ]

b) Kama jawabu ndio eleza kwa ufupi ni jinsi gani nahau za Kiswahili zinavyopelekea ugumu wa mawasiliano kwa wageni wa lugha hiyo.

_______________________________________________________________

5)Toa maani yako kuhusu matumizi ya nahau za Kiswahili jinsi zinavyosababisha kufeli kwa mawasiliano kwa wageni wa lugha.

**Ahsante sana kwa msaada wako. Allah akubariki**

## KIAMBATIHO Na 4

**MUONGOZO MASWALI YA MAHOJIANO KWA WALIMU**

Mpendwa mshiriki wa mahojiano haya Assalam alaykum

Maelezo kuhusu mtafiti Mimi ni mwanafunzi halali wa chuo kikuu huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya "Nahau za Kiswahili sanifu jinsi zinavyokwamisha Mawasiliano fanisi kwa Wageni wa Lugha." hivya naomba mashirikiano mema kutoka kwako kwako

**Taarifa binafsi za mtafitiwa**

1)Umri____________________________________________________

2)Mume_____________________________Mke________________________

3)Kiwango cha elimu anayofundisha : sekondari [ ]

Chuo

[ ]

4)Dhamana

Mwalimu [ ] Mwanafunzi [ ]

**Maswali**

1a) Je! Unazifahamu nahau za Kiswahili?

b)Taja nahau za Kiswahili sanifu angalau 5.

2) Eleza maana ya nahau ulizozitaja hapo juu kama zinavyotumika katika Kiswahili.

3) Eleza maana ya nahau ulizozitaja kwa kuzingatia maumbo yaliyounda nahau hizo.

4) Je! Unafikiri matumizi ya nahau za kiswahili yanaweza kukwamisha mawasiliano fanisi kwa wageni wa lugha?

5) Eleza kwa ufupi ni jinsi gani nahau za Kiswahili zinavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lugha hiyo.

6) Toa maoni yako kuhusu matumizi ya nahau za Kiswahili zinavyosababisha kukwama kwa mawasiliano kwa wageni wa lugha .

**Ahsante sana kwa mashirikiano yako mema. Allah akubariki**

**KIAMBATIHO Na 5**

**MUONGOZO MASWALI YA MAHOJIANO KWA WAGENI WA LUGHA**

Mpendwa mshiriki wa mahojiano haya Assalam alaykum

Maelezo kuhusu mtafiti Mimi ni mwanafunzi halali wa chuo kikuu huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya "Nahau za Kiswahili sanifu jinsi zinavyokwamisha Mawasiliano fanisi kwa Wageni wa

Lugha." hivya naomba mashirikiano mema kutoka kwako kwako

**Taarifa binafsi za mtafitiwa**

1)Umri___________________________________________________

2)Mume________________________________Mke_________________________

3) Dhamana

Daktari [ ] Mfanyakazi wakawaida [ ]

**Maswali**

1a) Je! Unaifahamu lugha ya kiswahili kwakiasi kikubwa?

b)Nitajie maneno yoyote katika lugha ya kiswahili unayohisi kwako ni magumu (huyafahamu).

2) Naomba nieleze maana ya maneno haya.

| MANENO | MAANA |
|---|---|
| Kuchimba dawa | |
| Amevunja chupa | |
| Amejifungua | |

3 Jee unapata shida yoyote wakati watumiaji wa lugha ya kiswahili wanapozungumza na wewe?

4 Toa maoni yako jambo gani lifanyike wakati wa shida inapokufikia kutokana na mazungumzo ya wenyeji wa lugha ya kiswahili.

**Ahsante sana kwa msaada wako. Mungu akubariki**